Date Printed: 04/23/2009

JTS Box Number: IFES_73

Tab Number: 1

Document Title: Nani Hupiga Kura Tanzania na Kwa Nini?

Document Date: 1995

Document Country: Tanzania

Document Language: Swahili

IFES ID: CE01886

*A3D6FEB7-2E23-4613-8E0B-679D3824BE75*

# NANI HUPIGA KURA TANZANIA NA KWA NINI?

T. L. Maliyamkono

EASTERN AND SOUTHERN AFRICAN UNIVERSITIES RESEARCH PROGRAMME

# NANI HUPIGA KURA TANZANIA NA KWA NINI?

Tema Publishers Company Ltd.,
Dar es Salaam

Kimechisaniwa na
Eastern and Southern African Universities
Research Programme
P.O. Box 35121, Dar es Salaam, Tanzania

©T. L. Maliyamkono 1995
Chapisho la Kwanza 1995

ISBN 9987 25 007 6

Kimetaipusetiwa na Kuchapwa na
Colourprint Limited,
P.O. Box 44466, Nairobi

## YALIYOMO


Vifupisho: .......... v
Orodha ya Grafu .......... v
Orodha ya Jedwali .......... v
Shukrani .......... vi
Utangulizi .......... vii

**SURA YA 1**

**1994: SEMINA ZA WALIMU WA WALIMU** .......... 1

1. Lengo .......... 1
2. Matukio Tangu Mkutano wa Arusha .......... 1
3. Mkutano wa Gaborone .......... 4

1.3.1 Mpango wa Mafunzo ya Walimu .......... 6
1.3.2 Uimarishaji wa Uwezo wa Kiutawala wa Vyama vya Kisiasa .......... 7
1.3.3 Ufuatiliaji wa Uchaguzi .......... 13
1.4. Mpango wa Elimu ya Uchaguzi Kura Tanzania .......... 15
1.4.1 Semina ya Kitaifa ya Walimu wa Walimu wa Elimu ya Uchaguzi .......... 17
1.4.2 Semina za Mafunzo Wilayani .......... 19
1.4.3 Semina za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali .......... 21
1.4.4 Maoni ya Washiriki wa Semina .......... 22

**SURA YA 2**

**ATHARI ZA MAFUNZO YA SEMINA ZA WALIMU** .......... 24

2.1 Athari Kamilifu .......... 24
2.2 Matukio Yaliyoingilia Athari .......... 24
2.3 Apathi .......... 28
2.4 Athari Halisi .......... 29
2.5 Mashaka ya Wanasemina Kuhusu Mtaala .......... 31
2.6 Maoni ya Wataalam Waendeshaji wa Semina .......... 32
2.7 Mkutano wa Kamati ya Utendaji Lusaka .......... 32
2.8 Kufunguliwa na Kufungwa kwa Semina na Maafisa wa Serikali .......... 33

**SURA YA 3.**

**UFAFANUZI WA SAMPULI YA WATOA HABARI** .......... 34

3.1 Sampuli .......... 34
3.2 Ufafanuzi wa Watoa Habari .......... 34
3.3 Vigezo Changanuzi (au Vibadala) .......... 37

**SURA YA 4**
**MATOKEO YA UTAFITI** ........ 43

4 Ufahamu wa Hatua za Uchaguzi ........ 43
4.1 Watu Wanavyopata Habari Kuhusu Kujiandikisha na Kupiga Kura ........ 43
4.2 Nani Anastahili Kuwa Mgombea katika Uchaguzi ........ 44
4.3 Jinsi Watu Wanavyojiandikisha Kupiga Kura ........ 44
4.4 Sababu za Kutojiandikisha Kupiga Kura ........ 44
4.5 Kwa nini Kuwa na Chaguzi za Mara kwa Mara ........ 44
4.6 Nini Huwavutia Watu Kupiga Kura ........ 45
4.7 Hatua za Uchaguzi Baada ya Uchaguzi Wenyewe Kumalizika ........ 47
4.8 Unafikiri ni kwa Nini Tumebalidilisha Mfumo wa Siasa Kutoka Mfumo wa Demokrasia ya Chama Kimoja Kwenda Kwenye Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi ........ 48
4.9 Maoni ya Jumla Kuhusu Elimu ya Demokrasia ........ 49

**SURA YA 5**
**MUHTASARI NA HITIMISHO** ........ 50
5.1 Maeneo ya Utafiti ........ 50
5.2 Muhtasari wa Matokeo Maalum ya Utafiti ........ 52
5.3 Vyombo Gani vya Habari Vyakutegemewa ........ 53
5.4 Kwa Nini Tanzania Imeingia Mfumo wa Vyama Vingi? ........ 54
5.5 Kuhusu Semina za Walimu wa Walimu ........ 54
5.6 Mapendekezo ........ 54

**Viambatisho:** ........ 56

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **CCM** | Chama Cha Mapinduzi |
| **CUSO** | Canadian Universities Services Overseas |
| **DC** | District Commissioner (Mkuu wa Wilaya) |
| **ELCT (KKKT)** | Evangelican Lutheran Church of Tanzania (Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania) |
| **EPPM** | Enhancement of Political Party Management |
| **ESAURP** | Eastern and Southern African Universities Research Programme |
| **FORD** | Forum for Restoration of Democracy |
| **MA** | Master of Arts Degree (Stashahada ya Pili) |
| **NEC** | National Electoral Commission (Tume ya Taifa ya Uchaguzi) |
| **NGO** | Non-Governmental Organisation (Mashirika yasiyo ya Kiserikali) |
| **NOVIB** | Netherlands Organisation for International Development |
| **OIC** | Organisation of Islamic Countries |
| **RC** | Regional Commissioner (Mkuu wa Mkoa) |
| **RDD** | Regional Development Director (Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa) |
| **TOT** | Trainers of Trainers (Walimu wa Walimu) |
| **TTVE** | Training of Trainers for Voter Education (Mafunzo ya Wakufunzi Elimu kuhusu Uchaguzi) |
| **UDP** | United Democratic Party |
| **UK** | United Kingdom |

## ORODHA YA GRAFU


Grafu 1 Sababu za Kupiga kura

Grafu 2 Watu Hupigia Nini Kura: Maswala

Grafu 3 Sababu za Kuwa na Chaguzi za mara kwa mara

Grafu 4 Njia za Kufahamu Hatua za Uchaguzi

Grafu 5 Sababu za Kuingia Mfumo wa Vyama Vingi

Grafu 6 Athari za mfumo wa Vyama Vingi

Grafu 7 Sababu za Kutojiandikisha kupiga Kura

Grafu 8 Watu Hupigia Nini Kura: Sifa za Binafsi


## ORODHA YA JEDWALI


Jedwali 1 Jinsia na Vibadala Vingine

Jedwali 2 Data Kuhusu Watu

Jedwali 3 Jinsia Kutegemea Makazi

Jedwali 4 Uzoefu Katika Kupiga Kura na Vibadala Vingine

Jedwali 5 Sababu za Kujiandikisha Kupiga Kura; Sababu za Kupiga Kura; Watu Hupigia nini Kura

Jedwali 6 Makazi: Dar es Salaam Dhidi ya Sehemu Nyingine za Nchi

Jedwali 7 Sababu za Kuwa na Chaguzi za mara kwa mara; Njia za kupata Habari kuhusu uchaguzi

Jedwali 8 Sababu za Kuingia Mfumo wa vyama vingi; Matokeo ya kuingia mfumo wa vyama vingi

# SHUKRANI

Watu wengi walitoa misaada mbali mbali katika vipindi tofauti vya utayarishaji wa kitabu hiki.

Natoa shukrani nyingi kwa wenzangu katika Sekretariati ya ESAURP ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wa mikataba na watafiti washiriki. Pia natoa shukrani kwa vikundi mbali mbali vya mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs), wachungaji na wafanyakazi wengine wa Kanisa, Maafisa wa Serikali ya Tanzania kwa kutusaidia kukamilisha taratibu na vibali tulivyohitaji kufanya kazi yetu; Walimu wa Walimu (TOT) waliowasaidia wafanyakazi wa ESAURP. Zaidi ya yote shukrani zinatolewa kwa Jumuiya ya Kimataifa ambayo ilitoa msaada wa fedha ya kuendeshea shughuli nzima (kama walivyoorozeshwa Kiambatisho husika). Vyombo vya habari vilitoa huduma nzuri sana kiasi kwamba sidhani kama hadhara imewahi kuelimishwa kuhusu kazi yangu nyingine yeyote vizuri kiasi hiki hapo nyuma. Nimeamua kuandika kitabu mwenyewe ili nibebe lawama zote na makosa yoyote yale bila kuwahusisha watu na Taasisi zote nilizotaja hapo juu kwa michango yao kwenye kufanikisha uchapishwaji wa kitabu hiki.

T.L. Maliyamkono
Januari 1995

# UTANGULIZI

Kwanza, kitabu hiki kinaelezea mpango wa ESAURP kuhusu Elimu ya Demokrasia. Pili, kinatoa muhtasari wa maoni ya waliohojiwa - walimu wa walimu na wakuu wenye kauli katika jamii kuhusu maswala muhimu yanayoambatana na mwenendo mzima wa demokrasia.

Kitabu kimelenga kwa wasomaji wa aina mbali mbali na siyo tu wanataaluma. Ni kijitabu kidogo cha vitendo kuliko nadharia chenye lengo la kuhimiza maendeleo mazuri ya mwenendo wa mabadiliko ya kidemokrasia nchini Tanzania, kwa kuanzia, na katika nchi zote za kanda ya ESAURP kwani mazingira yanafanana. Ni kijitabu kinachotarajiwa kutumiwa sana na wale walio katika mstari wa mbele katika kuwania nyazifa za kisiasa - hususan wale wanaotaka kupigiwa kura na wananchi kwa matarajio ya kutoa uongozi mzuri unaosaidia katika kuinua kiwango cha uzalishaji kiuchumi; wale wote ambao lengo lao ni kuinua ubora wa maisha ya wananchi.

Vyama vya kisiasa na wagombea viti vya kisiasa lazima waelimishwe kuhusu mambo yapi ni muhimu kutekelezwa ili mtu afanikiwe kupata cheo cha kisiasa. Ni lazima kuwaelimisha kuhusu vipi wangeweza wakaongeza uwezekano wa wananchi kuwaweka wao madarakani kwa kuwapa kura zao. Nyakati zimebadilika. Katika Uchaguzi Mkuu wa 1995 uchaguzi siyo tena wa kuchagua mmoja kati ya wagombea wawili wa chama kimoja kile kile. Uchaguzi ni mpana zaidi kuliko hapo nyuma.

Kuna swala la haki za binadamu kwa vile kila mtu mzima mwenye umri wa miaka 18 au zaidi, ambaye akili yake ni timamu, ambaye kwa wakati huo hatumikii kifungo cha ndani, na ambaye zaidi ya yote ni raia wa Tanzania, huyu mtu ana haki ya kupiga kura. Swala hili linagusia juu ya uhuru na haki za mtu binafsi kama inavyoelezwa na katiba ya nchi. Mtu kuelewa haki zake ni jambo moja, na ni jambo jingine kabisa kutenda mambo yanayolingana na uwelewa huo.

Ili kuweza kujua kwa vitendo hali ilivyo katika kushiriki uchaguzi, ESAURP ilifanya utafiti ili kutafuta kung'amua ni mantiki gani za kawaida (kile wanataaluma wanachokiita vibadala tegemezi) zinazotumika katika kujua kwa uhakika ni nani ambaye anategemewa kupiga kura. Vigezo au Vibadala hivyo ni pamoja na: umri wa mpiga kura, elimu yake, jinsia yake, ajira na kazi yake, anapoishi huyo mpiga kura (kama ni mjini au vijijini) ambapo Dar es Salaam pekee kwa minajili ya utafiti huu ndiyo inayohesabiwa kama mjini. Zaidi ya hapo, utafiti huu ulitafuta kubainisha ni kitu gani huwavutia wananchi kupigia mgombea fulani kura. Vigezo kadhaa vilipendekezwa kwa mpiga kura ikiwa ni pamoja na: ujuzi wa mgombea wa mbinu za kushawishi wapiga kura na ufahamu wake wa mambo yanayowakera wapiga kura; sura na maumbile ya mgombea, kabila lake, umri wake na uzoefu wake wa kisiasa. Pia kulikuwepo maswala kama mgombea kuwapa wapiga kura matumaini ya maisha bora siku za usoni; zawadi kama vile pesa wakati wa kampeni;

mgombea kutumia vitisho na mabavu, na mazoea (ukweli kwamba watu wanekuwa wakimpigia kura mgombea fulani, na wanataka kuendela kufanya hivyo.)

Kuhusu kwa nini watu hujihangaisha kupiga kura, utafiti ulitafuta kubainisha ikiwa jamii ya Kitanzania kweli imekomaa katika uwanja wa siasa kiasi cha watu wake kuweza kujua kuwa kupiga kura ilikuwa sehemu ya kutekeleza haki zao za kimsingi za kibinadamu na kuwa kutokufanya hivyo pia kulikuwa kielelezo cha utekelezaji wa haki zao za kibinadamu na wala haikukinzana na sheria yoyote. Tanzania, kujiandikisha kupiga kura na kupiga kura ni hiari na mtu halazimiki kujiandikisha kama ilivyo U.K., au hawajibiki kujiandikisha na kupiga kura kama ilivyo Australia. Ajenda iliyojificha ilikuwa kuchunguza ikiwa Watanzania wanahusianisha kati ya demokrasia ya vyama vingi na maendeleo ya kiuchumi.

Yapo maswala mawili yaliyojitokeza kuwa muhimu kipindi chote cha shughuli za utafiti. Maswali yaliulizwa kuhusu kazi ya Tume ya Uchaguzi, uhai wake kisheria, shughuli zake na madaraka yake. Pia ilionekana wazi kuwa ilihitajika kuwepo Maarifa ya njia madhubuti za kusambaza habari kuhusu haki za binadamu na maswala ya mwenendo wa demokrasia. Njia za kusambaza taarifa zilizopendekezwa zilikuwa pamoja na: redio, magazeti, semina na vijitabu, taarifa za mdomo kwa mdomo kupitia marafiki na ndugu pamoja na bila shaka taarifa kupitia mikutano ya kampeni za vyama vya kisiasa.

Mwisho, wahojiwa kwenye utafiti waliombwa kutoa tathmini kuhusu umuhimu wa semina za mafunzo kwa walimu, kwanza kabisa kama ni muhimu au hapana, na pili kama yanafaa kuendelezwa.

SURA 1

# SEMINA ZA WALIMU WA WALIMU - 1994

## 1.1 Lengo

Lengo la jumla la kuendesha semina za walimu wa walimu ilikuwa ni kujaribu kukabili suala la ususaji wa wapiga kura ambao umetawala sio tu katika jamii ambazo ni changa katika siasa za vyama vingi, lakini pia kwenye jamii zilizokomaa ambapo Serikali zinawekwa madarakani na asilimia 30 tu ya wapiga kura. Hali ni mbaya zaidi pale dhana potofu ya "mshindi achukue kila kitu" inapotawala. Sababu za kususia uchaguzi katika uchaguzi wa madiwani wa 1994 zimetolewa kwenye ukurasa wa 50-51.

Tanzania ina utamaduni wa uvumilivu ambao haukadiriki. Wakati mwingine hali hii inajionyesha kwa njia ya kususia na wakati mwingine kwa kutojali. Uchaguzi mdogo wa Kwahani, Ileje, Kigoma, na Igunga umeonyesha kuwa kwanza kulikuwa na kiwango kidogo cha kujitokeza cha wapiga kura na kisha kukawa na rekodi ya kuanguka katika idadi ya kura kwa chama tawala. Kule Kwahani chama tawala kilipata asilimia 89 lakini kule Igunga kura zikashuka hadi asilimia 53. Kuna watu wachache ambao wanaweza kuhusisha kiwango cha chini cha kujiandikisha na kukosekana kwa chombo kinachoweza kuchukua nafasi ya CCM katika kuwashawishi watu kujiandikisha na kupiga kura. Badala yake CCM inajitahidi kushawishi wanachama wake tu.

Sababu nyingine ya kuwa na semina ilikuwa ni kuendeleza kawaida ya zamani ya kuwa na uchaguzi wa kidemokrasia wenye amani. Nia ni kuepukana na mateso ya binadamu na aina zote za mateso ambayo yanatawala katika nchi kadhaa. Baadhi ya nchi hizo ni jirani zetu na hivyo huhatarisha amani Tanzania na kuipunguzia uwezo wake wa kubakia mfano na kisiwa cha amani. Zaidi ya hayo, semina hizi zilifanyika ili kutimiza lengo la ESAURP la kujenga uwezo wa binadamu nchini.

## 1.2 Matukio Tangu Mkutano wa Arusha

Maendeleo ya kihistoria ya matukio tangu mkutano wa Arusha wa vyama vya siasa katika kipindi cha mpito kuelekea siasa ya vyama vingi katika kanda uliofanyika mwezi June, 1993 ni muhimu katika kipindi hiki. Mkutano huo ulifanyika kwenye kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Arusha nchini Tanzania, kati ya tarehe 26 na 28 mwezi Juni, 1993.

Mkutano uliandaliwa baada ya ESAURP kugundua kuwa nchi nyingi katika kanda hii ya Mashariki na Kusini mwa Afrika sasa zimechagua mfumo wa vyama vingi vya siasa na serikali. Vyama vya siasa vilivyo madarakani na vile vya upinzani vilikuwa vinaogelea kwenye maji yasiyofahamika kwani nchi nyingi ambamo vyama hivyo vimo, zina historia ya kuwa na utawala wa chama kimoja ambapo vyama vingine vya siasa vilipigwa marufuku. Kwa hiyo, vyama kwenye nchi hizi vilikuwa vinajiingiza vyenyewe kwenye

utaratibu wa siasa wa vyama vingi bila kuwa na mbinu na uzoefu ambao ulikuwa unahitajika katika kujenga na kudumisha chama ambacho kinaweza kuunda serikali au kuwa kibadala cha serikali iliyo madarakani wakati fulani.

Haja ya kuwa na chama cha siasa chenye uwezo katika mfumo wa vyama vingi imesababisha kufikiria mambo kadhaa kama vile: usajili wa chama, uandikishaji wa wanachama, kuanzisha chama kwa ajili ya taifa zima, muundo wa chama, kuchangisha pesa, kutatua migongano ya ndani na matumizi ya vyombo vya habari. Mkutano ulizungumzia haya na masuala mengine chini ya mada za makala zilizotolewa. Makala hizo ni: Vyama vya Siasa, Demokrasia na Siasa ya Vyama vingi katika kanda yetu, Nafasi ya Vyama katika Jamii ya Kidemokrasia, Siasa za Chama na Taasisi za Dola, Muundo wa Kikatiba wa Vyama Vya Siasa katika Mfumo wa Vyama vingi, Matatizo ya Vyama Vya Siasa vilivyo Madarakani na vya Upinzani, Upigaji kura: Mbinu za vyama vya Siasa, vyama vya Siasa na Nafasi zao katika kuimarisha Uchaguzi Huru na wa Haki, Usimamizi wa Uchaguzi, Mfumo wa vyama vingi na Maendeleo ya Kiuchumi, na Uimairishaji wa Demokrasia. Kushiriki vizuri kwa wajumbe, kuliweka wazi uzoefu na matatizo ya vyama vya siasa katika jitihada zao za kujijenga kwa vyama vyenye uwezo wa kuunda serikali au kuwa wapinzani imara.

Mkutano ulipata mahudhurio mazuri. Kulikuwa na vyama vya siasa 31 kutoka nchi 9 na washiriki kutoka nchi 17.

Uchangiaji mawazo katika mkutano ulikuwa mkubwa na katika mazingira mazuri. Wingi na ubora wa washiriki unaweza kuthibitishwa na idadi kubwa ya makala za mkutano ambazo zilikuwa 34 kwa ujumla. Makala 28 kati ya hizo zilihudhurishwa na vyama vya siasa vyenyewe.

Ni wazi kuwa, lengo kubwa la mkutano ambalo lilikuwa kuwaleta pamoja viongozi wa vyama vya siasa (vinavyotawala na vya upinzani) katika nchi za kanda yetu lilifikiwa kwa kiasi kikubwa. Nia ilikuwa ni kujadili na kupeana uzoefu na mawazo katika mazingira ya kirafiki na yasiyo ya upande wowote kuhusu masuala mbalimbali ya kinadharia na kimatendo ambayo yanajaribu kuzuia au kuendeleza kipindi cha mpito cha amani. Maoni yangu binafsi katika utangulizi wa kitabu kiitwacho The Cost of Peace 1994 bado yana maana:

> Kwa kuangalia kiwango cha uwakilishi wa vyama vya siasa na kwa ubora wa makala na maoni ambayo yalitolewa wakati wa majadiliano, mkutano usingeweza kuwa bora zaidi ya hapo. Kitendo cha kuwaleta pamoja wanasiasa wa vyama vya siasa vinavyopingana, hiyo peke yake ilikuwa ni alama ya ushindi wa mkutano. Hata hivyo kulikuwa na maana zaidi ya hapo. Mkutano ulikuwa na utulivu na wa kidemokrasia. Kwa mfano, vyama vyote vya siasa vya Tanzania ukiondoa chama tawala (CCM) na Tanzania People's Party, vilitoka nje ya ukumbi wa mkutano kwa amani wakati wa hotuba ya mgeni rasmi ili kuelezea hisia zao. Kwa watu wengine suala hili lilionekana kama kitendo cha kutumia "haki za kidemokrasia", wakati watu wengine waliona kuwa ni kukosekana kwa uzoefu na uvumilivu.

Ujumbe wa vyama vya siasa vya Kenya, Uganda na Botswana, japo vilianza katika mazingira ya uhasama sana, waliweza kuendelea kubaki katika ukumbi mmoja, kushikana mikono, na kuheshimu maoni ya mwingine bila kulazimika kupata mwafaka au kutupilia mbali msimamo wao.

Mafanikio makubwa ya mkutano yanaonekana katika maazimio yake. Vyama vya siasa 31 kutoka nchi 10 tofauti viliweza kuweka msimamo wa kulaani utawala wa Kijeshi wa Nigeria kwa kutengua matokeo ya uchaguzi; kulaani Ufalme wa Swaziland kwa kuingilia kati zoezi la kuleta demokrasia; kumsifu Banda wa Malawi kwa kukubali maendeleo ya misingi ya vyama vingi; kumlaani Savimbi wa Angola kwa kushindwa kukubali kushindwa uchaguzi na kuanzisha tena mapigano; na kutoa wito wa nguvu za pamoja za kujenga chombo cha kanda ambacho kitatoa huduma za baadaye za kanda ili kuendeleza demokrasia. Mkutano ulipata mwafaka muhimu.

Mwishowe, kulikuwa na maendeleo ya kisiasa yaliyotokana na mkutano mara tu baada ya kufungwa kwake. Kitendo cha kutoka nje ya ukumbi kwa vingi ya vyama vya siasa vya Tanzania katika mkutano cha kumpinga Salmin Amour, kilichochea maandamano makubwa huko Zanzibar. Ujumbe ulikuwa yeye alikuwa mwana halisi na mtawala wa Zanzibar na sio dikteta kama vyama 9 vya siasa vya Tanzania vilivyodai. Katika Ufalme wa Swaziland, wawakilishi wa vyama viwili vya upinzani walihojiwa walipotua kwenye uwanja wa ndege. Kamati kuu ya chama cha Mapinduzi (CCM) na FORD KENYA zilijadili majadiliano yaliyofanyika katika mkutano na athari za maazimio ya mkutano mara tu baada ya mkutano kufungwa. Vyombo vya habari vya Tanzania viliutangaza sana mkutano huu. Kwa pamoja, kulikuwa na zaidi ya makala 19 katika magazeti katika miezi 2 iliyokizunguka kipindi cha mkutano nchini Tanzania. Zaidi ya hapo gazeti la Zambia liitwalo Development Dialogue limechapisha makala ndefu kuhusu mkutano. Shirika la utangazaji la BBC na Redio Tanzania zilitangaza masuala yaliyojitokeza kwenye mkutano.

Yote haya yaliongeza uzuri katika kushiriki kwenye mkutano uliotayarishwa hasa kuamsha utambuzi wa kisiasa katika umma wa vyama vya siasa unaoelekea kwenye demokrasia ya Afrika.

Kulikuwa na mapengo ya wazi wakati wa mkutano ambayo yalitokana na kushindwa kwa ujumbe wa vyama vya siasa kuelewa masuala ambayo yalikuwa ya msingi katika mada za mkutano. Kwa mfano vyama vya siasa vilitilia maanani zaidi maeneo yale ambayo vyama tawala havifanyi vizuri, na ugumu wa kuingia kwenye madaraka. Kwa upande mwingine vyama tawala vililaumu vyama vya upinzani kwa kukosa mwelekeo.

Muda mwingi huko Arusha ulitawaliwa na majadiliano kuhusu njia na uwezo wa kuthibiti vyombo vya dola, masuala ya pesa na kukubalika kwa vyama. Mkutano ulitoa ushahidi wa kutosha wa mambo ambayo hayajapatiwa ufumbuzi katika kipindi cha mpito kuelekea kwenye demokrasia ya vyama vingi. Mambo haya ni pamoja na kushindwa kutenganisha kati ya kazi za serikali na kazi za chama cha siasa; kutokuwa na chama cha upinzani madhubuti; migongano ya ndani na utengano. Zaidi ya hayo, hisia za undani zilitolewa kuwa, zile nchi zinazojulikana kama nchi asilia za demokrasia ya vyama vingi sio lazima kuwa ni nchi za kidemokrasia.

Mkutano wa Arusha ulidai chombo cha kanda kiundwe ili kuendeleza demokrasia na kuiomba ESAURP kuandaa utaratibu sio tu wa kuunda taasisi bali kubuni kazi zake pia. Azimio Na. 11 la mkutano linasema hivi:

> Kuanzisha kamati ya kanda ya demokrasia na utawala ambayo itakuwa na vyama vya siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za elimu ya juu. Mkutano uliazimia pia kwamba

ESAURP baada ya kubeba azima hii inatakiwa pia ibebe mzigo wa uongozi katika uundaji wa kamati hiyo ambayo itaunda mpango wa utafiti na mafunzo katika ngazi ya kanda katika masuala yanayohusu demokrasia na utawala. Mkutano uliazimia kuwa shughuli za kamati zigharimiwe na Serikali za kiafrika na jumuiya ya kimataifa inayopenda kuendeleza demokrasia barani Afrika.

Kati ya June 1993 na Januari 1994, Sekretarieti ya ESAURP ilibidi kurekebisha mpango wake ili kuingiza kazi yake mpya: kuwa mwenyeji wa Sekretarieti ya kuratibu ambayo itafanya kazi katika utaratibu uliopendekezwa na mkutano wa Arusha yaani kusimamia maendeleo ya kisiasa katika kanda ya ESAURP. Kazi zifuatazo ziliundwa: kuhariri makala za kuchapisha kitabu (The Cost of Peace); kuandaa Rasimu ya Miradi ambayo litajadiliwa kwenye mkutano wa Gaborone (Rasimu ya Mradi wa Elimu ya Demokrasia) na kuchangisha pesa.

## 1.3 Mkutano wa Gaborone

Matayarisho ya mkutano yalikamilika mwishoni mwa mwaka 1993 na ilipofika Januari, 1994 mkutano ulifanyika mjini Gaborone, Botswana.

Mjini Gaborone, nchi 9 kati ya nchi 12 za ESAURP zinazoshiriki kwenye mpango huu, ziliwakilishwa na makundi mawili ya wanasiasa. Kwa upande mmoja kulikuwa na wawakilishi wa vyama vya siasa vinavyotawala na kwa upande wa pili kulikuwa na wawakilishi wa vyama vya upinzani, ambavyo hujulikana kama vyama vipya vya siasa. Baraza la uwakilishi la makundi hayo mawili liliundwa (angalia jarida la Baraza la Demokrasia 1994) Mkutano ulizungumzia masuala manne muhimu: maadili ya kitaifa, uhusiano kati ya demokrasia na maendeleo ya kiuchumi, msimamo wa jumuiya ya wafadhili kuhusu demokrasia katika Afrika, na kugharimia mpango wa Baraza.

a) Katika hotuba yake kwa mkutano, Waziri wa Nchi wa Mipango wa Tanzania, Bwana Horace Kolimba alisema kuwa kuna haja ya kuwa na maadili ya kitaifa kwa kila nchi, maadili yaliyokubaliwa na vyama vya siasa. Alisema:

> "Dhana ya "Maadili ya Taifa" lazima ikubaliwe na wote kwa sababu ni kwa manufaa ya wote." "Maadili haya ya Taifa" ambayo ni pamoja na kukataa matumizi ya mabavu kama njia ya kupata ushindi wa utawala au kushinda hoja. Sheria za haki za uchaguzi, kushiriki kwenye uchaguzi huru na wa haki iwe ndio njia halali ya kushika madaraka ya Serikali. Zaidi ya hayo, vyama vya siasa Afrika lazima vikubali matokeo ya uchaguzi huru wa haki badala ya kutafuta visingizio vya kuyakataa.

b) Mkutano wa Gaborone ulihisi kuwa kuna uhusiano kati ya maendeleo ya kiuchumi na demokrasia ya vyama vingi lakini ulishindwa kuwa wazi kuhusu uhusiano huu. Suala hili lilijitokeza kutokana na maoni ya utangulizi aliyoyatoa Balozi wa Marekani Howard Jeter kwenye mkutano:

> Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya demokrasia na maendeleo, mambo haya mawili hutegemeana, na kuleana, na kwa pamoja kuzaa kitu kikubwa kwa idadi kubwa. Inawezekana

kuwa na maendeleo ya kiuchumi bila demokrasia lakini sio kwa kipindi kirefu. Serikali zisizo za kidemokrasia hujifungia, hujilinda na haziwajibiki kwa raia zake na kwao wenyewe. Ni meneja wabovu wa kijamii na hawana ubunifu. Serikali zisizo za kidemokrasia huchanganya nia na ubunifu wa watu wake na hupenda kukiuka haki za msingi za binadamu na uhuru. Mara tu hupoteza kukubalika na hufa. Haziwezi kudumisha kuungwa mkono na watu wake.

c) Tabia ya kutofungamana na upande wowote wa taasisi zinazoendeleza demokrasia ilipokelewa kwa shangwe kubwa. Niliuambia mkutano kuwa:

> Sio tu tusifungamane na upande wowote, bali pia ni lazima tuonekane hatufungamani na upande wowote. Ni kwa sababu hii ndio ninataka tuelezane nanyi mashaka ambayo sisi, kama taasisi, tunajikuta tunayo wakati tunapojaribu kutekeleza kazi za mradi.
>
> Mipango ya kanda na mikutano haiwezi kuendeshwa bila ushirikiano wa serikali. Kwa hiyo, ni wajibu wetu kufanya kazi karibu sana na vyama vya siasa vinavyotawala, kama mpango wa kanda uliopendekezwa unatakiwa ufanikiwe. Kwa hiyo kuna hatari kuwa ESAURP inaonekana na vyama vya siasa vya upinzani kama inafungamana na serikali. Wakati huo huo, kwa ajili ya kushiriki katika mkutano na kuupa uhalali mkutano na mipango ya kuleta demokrasia ni lazima tufanye kazi karibu sana na vyama vya upinzani.
>
> Kwa mfano, bila uwakilishi wa vyama vya upinzani katika Mpango wa Taifa wa Elimu ya wapiga kura, mpango unaweza ukaonekana kama propaganda ya serikali. Kwa hiyo, tunakubali kukosolewa kwa upande mmoja kutoka vyama vya siasa vinavyotawala kwa kutofungamana navyo na kwa upande mwingine kutoka kwenye vyama vya upinzani kwa kuonekana kuwa tunaisaidia serikali. Ni lazima nisisitize kuwa, agenda yetu ni kubaki tusiofungamana na upande wowote kabisa na kwamba kama shirika lisilo la kiserikali tunazo sifa za kuifanya kazi hiyo.

d) Suala la kugharimia mradi lilikuwa suala muhimu katika mkutano, baada ya wajumbe kugundua kuwa itakuwa vigumu kwa serikali za Kiafrika kugharimia mradi huu hasa katika hatua zake za mwanzoni. G. Chiepe, Waziri wa Nchi za Nje wa Botswana alisema katika hotuba yake ya ufungaji wa mkutano kuwa:

> Mnahitajika kuchangisha pesa ili kutekeleza mipango ya elimu ya kupiga kura, uwezo wa kiutawala wa vyama vya siasa na usimamizi wa uchaguzi. Hii ni sehemu ngumu na muhimu sana katika kazi yenu. Lazima mzingatie suala la kuchangisha pesa kwa nguvu na moyo kwa sababu utekelezaji wa mipango yenu ya sasa na baadaye itategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa fedha.

e) Na Howard Jeter aliweka msisitizo kwenye utendaji wa baadaye wa Jumuiya ya Wafadhili katika kujaribu kuendeleza demokrasia.

Alisema:

> Marekani imesema wazi kuwa nchi zile ambazo zinaonyesha kutenda kwa dhati na kwa kuendelea kuhusu demokrasia zitapata kipaumbele cha misaada ya Marekani. Kwetu sisi hizi sio jitihada za kutenda wema na vita baridi vya mashindano ya kiitikadi vimekwisha. Tunasaidia demokrasia kwa sababu ni kwa manufaa ya Taifa letu kufanya hivyo. Ni jambo sahihi kufanya hivyo. Sio jukumu la Marekani na wala sio kwa maslahi ya Marekani kujaribu kuamua nani aitawale nchi yoyote ya Afrika. Hatutaingilia uchaguzi wowote wa Afrika.

Uchaguzi ni suala la watu kuamua. Japokuwa wakati fulani tutaonekana kukosa uvumilivu, Amerika inatambua kwamba demokrasia ya kweli inachukua muda kuijenga, na kwamba hata baada ya muda kupita, matokeo yanaweza yasiwe kamilifu. Tunachotaka kupata ni uthibitisho kuwa serikali zinafanya jitihada za dhati na za kuendelea kuelekea kwenye mwelekeo sahihi. Kuheshimu haki za binadamu, kuanzisha mazungumzo ya maana ya kisiasa, kuwa wakweli na wazi katika serikali na kusaidia jamii huru. Serikali zinazofanya kazi kwa nia ya kufikia malengo haya zinaweza kutegemea na zitapata msaada wa Marekani. Serikali ambazo zinakataa mageuzi haya zisitegemee ushirikiano wetu wa kikamilifu. Hili sio tishio wala adhabu, bali ni tamko tu la hali halisi ya sasa.

Lakini ili kuipendeza Marekani serikali za Kiafrika zifanye mageuzi ya kidemokrasia. Zikifanya kwa faida yao, nchi ambazo zitakubali demokrasia zitaendelea, zitasitawi na kukua. Nchi hizi zitakuwa na amani na utulivu. Kwa pamoja, nchi hizi za kidemokrasia zinaweza kutatua matatizo ya Afrika na Bara hili litatoa mchango mkubwa ulimwenguni. Jambo hili ndilo linalohitajika kwa Afrika. Na hili ndilo jambo ambalo Amerika inahitaji kwa Afrika. Tutawaunga mkono kwa vile tunawatakia kheri.

Ili kufanya kazi, Baraza lilihitaji ushirikiano kamili wa ESAURP kama Taasisi kuunda Sekretarieti, na kupanga kazi za Baraza, na kusaidia katika kuchangisha pesa na utawala. Afisa Mafunzo Mkuu aliteuliwa kuwa mjumbe wa Sekretarieti ambayo itafanya kazi chini ya kamati ya utendaji ya wajumbe 10 wa Baraza. Kwa ufupi, Baraza liliunda nguvu zake, likaweka mipaka ya utawala wake na kuelezea kazi zake kwa kulenga Elimu ya Demokrasia ambayo itatolewa kwa kupitia mipango mitatu: Mafunzo ya walimu, Uimarishaji wa uwezo kiutawala wa vyama vya siasa, na Usimamizi wa Uchaguzi.

### 1.3.1 Mpango wa Mafunzo ya Walimu

Mpando huu ulianzishwa ili kushughulikia Elimu ya kupiga kura. Malengo manne yaliwekwa:

Kufunza walimu na viongozi wa maoni ambao watafanya kazi kama walimu katika nchi zao kuuelezea umma juu ya haki za kupiga kura na wajibu, uandikishaji na mbinu za uchaguzi.

Kuinua kiwango zaidi cha kuelewa miongoni mwa wapiga kura kuhusu wajibu wao katika zoezi la kidemokrasia ili kuwafanya washiriki zaidi kwenye kupiga kura na kuwa na mshikamano wa muda mrefu wa kuleta demokrasia.

Kuhimiza na kusaidia kushiriki kikamilifu kwa wanawake, kama walimu au wanafunzi katika mafunzo ya walimu wa mpango wa Elimu ya kupiga kura.

Kupata data ya utafiti kwa kupitia viongozi wa maoni hususani maoni ya wapiga kura juu ya uhusiano kati ya ujenzi wa demokrasia na maendeleo ya kiuchumi, ambayo baadaye data hiyo inaweza kutumiwa katika kazi za utafiti wa uandani za shahada za juu na mpango wa kunoa ubongo.

### 1.3.2 Uimarishaji wa Uwezo wa Kiutawala wa Vyama vya Siasa

Eneo hili la mafunzo lina sehemu 4

- Mafunzo kwa watumishi wa vyama vya siasa
- Mipango ya Utafiti wa uandani wa shahada za juu katika siasa, Demokrasia na utawala
- Mipango ya kunoa ubongo ya kanda
- Mikutano ya kanda

#### 1.3.2.1 Mafunzo kwa Watumishi wa Vyama vya Siasa

Mifumo ya kisiasa ya vyama vingi yenye mafanikio hutegemea kuwepo kwa vyama vya siasa imara vyenye uwezo wa kuunda serikali imara. Mpango unaokusudiwa umelengwa kwenye kuongeza uwezo wa kiutawala wa vyama vya siasa kitu ambacho ni sifa muhimu kwa chama chochote kinachotaka kuendesha shughuli za kisiasa kikamilifu, zenye mkusanyiko wa matakwa na haja ya kuelezea matakwa yao. Vyama vya siasa vinavyotawala na vile vya upinzani lazima vipangwe vizuri na viendeshwe vizuri kama vinataka kushindana kwa mafanikio katika nyanja za kidemokrasia, na kwa hali hii kunahitajika kuundwa kwa watumishi wenye jicho kali na walioandaliwa vizuri.

Mpango utasaidia upanuzi wa uwezo wa kiutawala wa vyama vya siasa kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wa vyama vya siasa katika makundi mawili.

a) Watoa maamuzi na Mameneja
b) Watumishi wa Kitaalamu

Kwa kuwa mahitaji ya kikazi kwa makundi haya mawili ni tofauti, mafunzo ya aina mbili tofauti yatatolewa katika mpango huu.

**i) Mafunzo kwa Watoa Maamuzi wa Vyama vya Siasa na Mameneja**

Sehemu ya kwanza ya mpango wa uwezo wa kiutawala wa vyama vya siasa utatolewa kwa kuzingatia mahitaji ya watumishi wa vyama halali au vilivyoandikishwa. Watu hawa ni pamoja na Katibu Mkuu, Mameneja wa Chama, Makatibu Wasaidizi, Wakurugenzi wa Idara na Wajumbe wa Kamati Kuu.

Mpango huu umeandaliwa ili kuwekeza katika rasilimali muhimu ambayo ni watumishi wa chama cha siasa katika kada za uongozi na menejimenti na hivyo kukijengea chama uwezo wa kiusimamizi.

Madhumuni ya mpango huu ni:

a) Kuhakikisha kwamba viongozi na mameneja wa Chama wanapata ujuzi juu ya uundaji, itikadi, utambulisho, muundo na utaratibu wa chama.

b) Kueneza mbinu za utayarishaji wa sera za chama, ilani za kampeni, na mbinu za uandaaji na usimamiaji wa mikutano ya kampeni.

c) Kuimarisha demokrasia na kujenga mbinu za kusuluhisha migogoro ndani ya chama.

d) Kuonyesha mbinu na manufaa ya vyombo vya habari vya umma na vya binafsi, katika uchaguzi.

e) Kueleza tatizo la kueleweka kwa masuala ya kisiasa miongoni mwa wapiga kura na jukumu la msingi la vyama vya kisiasa la kuwaelimisha wapiga kura kwa kuwajenga kisiasa.

f) Kueleza mbinu za kutafuta kuungwa mkono, hasa kwa njia ya fedha, na wananchi kwa ajili ya ujenzi na uhai wa chama.

g) Kurahisisha ubadilishanaji wa mawazo na uzoefu miongoni mwa viongozi wa chama wakati wakishiriki katika semina na kongamano zilizomo kwenye mpango huu.

h) Kueneza, kwa mapana ya kutosha, taarifa na maarifa yaliyotokana na mipango ya uzamili, ya kunoa ubongo na ya elimu ya uchaguzi miongoni mwa wanasiasa wa ngazi ya juu. (mipango hiyo imefafanuliwa huko mbele katika kitabu hiki).

i) Kuwapatia viongozi wa chama wanaohudhuria mafunzo mbalimbali, mbinu na maarifa vitakavyowawezesha kuwafunza wanachama wenzao ambao hawakupata mafunzo hayo.

j) Kuwaelimisha mameneja wa chama juu ya misingi ya sheria ya uchaguzi, kampeni, mwongozo wa mgombea,na udumishaji wa muundo wa chama katika vipindi vya kati ya chaguzi.

k) Kujenga utamaduni wa kuvumiliana kisiasa na wa kuzingatia kanuni, kawaida, na matendo ya kidemokrasia yaliyokubalika.

**Mpango wa Kozi**

Mpango wa kozi unajumuisha mada kama vile, maana halisi ya demokrasia ya vyama vingi, majukumu ya vyama vya siasa, utaratibu na muundo wa chama, utafutaji wanachama, mbinu za utayarishaji wa sera na miongozo ya chama, mbinu za uboreshaji mapato ya chama, uimarishaji na uoainishaji wa matakwa mbalimbali na utatuzi wa mgogoro.

Elimu ya uchaguzi hupelekea kuongezeka kwa uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa kwa vile huwahamasisha wapiga kura juu ya sera na majukumu ya vyama vya siasa. Aidha

data za utafiti zilizotokana na mawazo ya viongozi juu ya kiwango cha elimu ya mpiga kura yanaweza yakatumiwa kuunda kitengo cha data kwa ajili ya mipango ya uzamili na ya unoaji ubongo juu ya maoni ya wananchi kuhusu uhusiano baina ya demokrasia na maendeleo ya uchumi pamoja na mambo mengine yanayohusiana. Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa, kwa maana nyingine, kunapelekea kupanda kwa viwango vya elimu ya mpiga kura kwa vile ili vyama vya kisiasa vifanye kazi kikamilifu sharti vijihusishe na kuwajenga watu kisiasa.

Mipango ya kuimarisha uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa inahitaji vifaa na mbinu za kufundishia ambavyo vyote vitatokana na mipango ya uzamili na ya unoaji ubongo. Kwa upande mwingine mpango wa mafunzo kwa viongozi na mameneja wa chama utaibua masuala ya kinadharia na kiufundi ambayo yanaweza kutafitiwa na kuzungumziwa katika mipango ya mafunzo ya uzamili na ya kunoa ubongo.

Hivyo basi mpango wa mafunzo kwa viongozi na mameneja wa chama ni sehemu ya miradi mingi inayokamilishana na ambayo kwa ujumla wake itaashiria hatua moja kubwa mbele katika elimu ya demokrasia katika kanda hii.

Katika kutimiza lengo hili sehemu ya pili ya mpango wa uimarishaji wa uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa inahusu mahitaji maalum ya watumishi wataalam na kozi zao ndani ya muundo wa chama cha kisiasa. Waamuzi na mameneja wanahitaji watawala wasaidizi waliofunzwa vyema ili waweze kuzitenda kazi zao ipasavyo.

**ii) Mafunzo kwa Ajili ya Watumishi Wataalam wa Chama cha Siasa**

Sehemu ya pili ya mpango wa kujenga uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa umeelekezwa katika mahitaji ya kiujuzi ya wafanyakazi wataalam ambao hukiwezesha chama cha siasa kuendesha mambo yake kulingana na taratibu na kwa ufanisi.

Kozi za mafunzo maalum katika Sekretarieti ya ESAURP hutolewa kwa wafanyakazi wataalam wa vyama vya siasa vinavyokubalika kisheria na vilivyoandikishwa hasa kwa wafanyakazi wa chama cha siasa wanaojihusisha na kozi za utumishi na za kuandikisha wapiga kura, uhasibu, utawala kwa jumla na kozi za ukarani.

Madhumuni ya mpango huu ni:

a) Kuanzisha teknolojia ya habari ikiwa ni pamoja na mafunzo ya "micro-computing" na "word processing" kwa wafanyakazi wa Utawala.

b) Kutoa mafunzo juu ya matumizi ya mifumo ya kisasa ya kompyuta na uhifadhi data kwa ajili ya utawala na usimamizi wa fedha katika chama cha siasa.

c) Kurahisisha matumizi ya kompyuta katika maeneo kama vile ya idadi ya watu, kura ya maoni, matokeo ya kura na uundaji wa sera.

d) Kutumia ipasavyo (bila kufuja mali) vifaa vingi mbalimbali vya kompyuta katika ESAURP pamoja na watumishi wake wenye ujuzi katika kutoa mafunzo kwa idadi kubwa iwezekanayo ya wafanyakazi watawala.

e) Kurahisisha ubadilishanaji wa mawazo na uzoefu baina ya washiriki kwenye kozi wakati wa mafunzo.

f) Kuhamasisha mbinu ya utatuzi wa matatizo kwa pamoja na ya mawasiliano ya pamoja miongoni mwa wafanyakazi wa utawala kutoka katika vyama mbalimbali vya siasa katika kanda hii.

Mpango unaonyesha matumizi maalum ya mifumo hii kwa ajili ya wafanyakazi wataalam wa chama cha siasa, kwa mfano, unaonyesha namna ya kuanzisha hifadhi ya data kwa ajili ya uandikishaji wa chama na matumizi ya hifadhi ya data katika upimaji ukubalifu wa sera.

### 1.3.2.2 Mpango wa Mafunzo ya Uzamili katika Siasa Demokrasia na Utawala

Mpango huu unaanzishwa katika nchi za ESAURP zenye idara zilizokomaa za siasa katika chuo kikuu. Mafunzo ya utafiti yanayotolewa yatakuwa kwa ajili ya wanafunzi wa shahada ya uzamili(M.A) na stashahada, ambao baada ya kumaliza sehemu ya mafunzo ya darasani ya kozi yao ya siasa, demokrasia na utawala watafanya utafiti juu ya masuala yanayohusu uenezaji wa demokrasia.

Mpango huu una malengo manne yanayofungamana.

a) Kuunga mkono tafiti za kigunduzi ambazo hutoa taarifa kwa ajili ya masuluhisho ya papo kwa papo ya matatizo yanayohusiana na uenezaji unaofaa wa demokrasia na vyama vingi katika mazingira ya kiafrika.

b) Kuunda utaratibu wa usambazaji wa matokeo ya utafiti yaliyochapwa na serikali, vyama vya siasa na makundi mengine yanayopenda.

c) Kuunda bodi ya vitendo ya kufaa ya utafiti ambayo inaweza kuwa sehemu muhimu katika mafunzo kwa walimu kwa ajili ya Elimu ya uchaguzi na pia katika uimarishaji wa uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa; mipango iliyopendekezwa mwanzoni mwa kitabu hiki.

d) Kupanua moja kwa moja uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa katika vyama vya siasa vya eneo hili tukitilia maanani uwezekano wa baadhi ya wanafunzi katika mpango huu kupatiwa nafasi ya kutoa ushauri au ya majukumu mengine ndani ya chama na serikali.

Pamoja na kwamba ESAURP na Baraza la Demokrasia zinatambua mpango huu unatoa nafasi chache tu (nafasi 60 kwa mwaka) inatarajiwa kuwa mpango huu utakuwa na

manufaa makubwa kijamii kuliko yale ya kibinafsi watakayoyapata wale waliopata nafasi hizo chache.

Hakika pendekezo la utafiti linalokubalika ni lazima lidhihirishe kwamba pamoja na utafiti huo kumnufaisha mtafiti pia matokeo yake (tasnifu) yatakuwa na manufaa katika mipango yote miwili ya mafunzo kwa walimu wa elimu ya uchaguzi na uimarishaji wa uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa na katika maendeleo ya demokrasia ya vyama vingi na uenezaji wa demokrasia katika kanda hii ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Aidha inatarajiwa kwamba baadhi ya wanafunzi wanaomaliza mafunzo watafanya kazi katika nyanja zinazohusiana na siasa na hivyo kupelekea kuweko kwa ongezeko kubwa la uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa katika kanda hii. Matokeo yanayotarajiwa ni pamoja na:

a) Kutunga na kusambaza maandishi mbalimbali ya utafiti yenye manufaa ya moja kwa moja kimatumizi katika elimu ya uchaguzi na upanuzi wa uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa.

b) Kuendeleza maarifa katika nyanja za uenezaji demokrasia na vyama vingi kwa matarajio kwamba maarifa hayo yataingizwa na kutumiwa kwa ajili ya manufaa ya vyama vyote vya siasa vinavyopendwa na wapiga kura katika kanda ya ESAURP.

c) Upanuaji wa uwezo wa utafiti katika eneo hili hasa ule wa utafiti wenye manufaa katika masuala yanayohusiana na uenezaji wa demokrasia.

### 1.3.2.3 Mpango wa Kanda Unoaji Ubongo

Mpango huu unawapatia wahadhiri na watafiti wa eneo hili nafasi za kufanya utafiti katika sekretarieti ya ESAURP kwa kipindi cha miezi 3 hadi 12.

**i) Washiriki**

Mpango wa kunoa ubongo umebuniwa kwa ajili ya wanataaluma ambao nyanja zao za kitaaluma na tafiti walizopendekeza zinahusiana hasa na hatua za elimu kwa ajili ya kueneza demokrasia katika kanda ya ESAURP. Utafiti unatarajiwa hasa ushughulikie eneo muhimu la elimu ya uchaguzi na la mafunzo ya vyama vingi na uenezaji demokrasia kwa serikali na vyama vya siasa.

**ii) Malengo**

a) Kuhimiza na kuwasaidia watafiti wazamili katika kufanya tafiti ambazo zinatoa ufumbuzi wa moja kwa moja wa tatizo la elimu na mafunzo kwa ajili ya kueneza demokrasia.

b) Kuwapatia watafiti kutoka kanda ya sekretariati ya ESAURP nyenzo nyingi za kazi kutoka Sekretariati ya ESAURP ambazo ni pamoja na: watafiti wenye uzoefu,

vifaa vya kisasa kwa ajili ya upembuzi na uchanganuzi wa data, machapisho ya utafiti na kitengo cha data, ofisi, nyumba za kuishi kwa kuzingatia matumizi bora ya rasilimali chache za utafiti.

c) Kuimarisha sekretarieti ya kanda ya ESAURP kwa kuhimiza ushirikiano wa karibu wa Kimataifa na mawasiliano miongoni mwa wanataaluma wanaofanya kazi katika nyanja za utafiti zinazohusiana na mkondo mwafaka wa uanzishaji wa vyama vingi kwa njia ya elimu na mafunzo.

d) Kutoa mafunzo juu ya mbinu za kisiasa za utafiti, mbinu za uchanganuzi na vifaa vya ukadiriaji kitakwimu ambavyo kwa sasa vinapatikana katika sekretarieti (tazama mpango wa kozi wa ESAURP).

Kwa kujenga kituo cha utafiti cha kufaa na chenye rasilimali za utafiti za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa miradi ya kitaaluma katika maeneo ya uenezaji demokrasia, malengo yafuatayo yatafikiwa:

a) Uchapishaji na usambazaji wa ripoti za utafiti zinazohitajika na zinazofaa zitakazonufaisha serikali, vyama vya upinzani na wapiga kura na ambazo pia zinaweza kutumika kikamilifu katika mipango ya uimarishaji wa usimamizi wa chama cha siasa na utoaji mafunzo kwa walimu wa Elimu ya Uchaguzi (mipango ambayo imefafanuliwa katika kitabu hiki).

b) Kujenga na kuimarisha wataalam wa elimu ya uenezaji demokrasia katika kanda.

c) Kuanzisha kitengo cha data na maandishi ya utafiti kwa hali hiyo kusaidia katika kuongeza uwezo wa utafiti katika mada zinazohusiana na siasa.

d) Kuinua kwa kiwango kikubwa mawasiliano na ubadilishanaji wa mawazo, matokeo ya utafiti na uzoefu katika maeneo ya elimu kwa ajili ya kueneza desturi, dhana na mazingira yanayotakiwa ya demokrasia.

e) Matumizi kamilifu ya vifaa vya mafunzo na utafiti vya sekretarieti ya ESAURP kwa lengo la uchangiaji kikamilifu kwa pamoja wa rasilimali chache za utafiti na la usambazaji wa mbinu za utafiti za kisiasa.

### 1.3.2.4 Vikao Vya Kanda

Kutakuwa na kikao cha viongozi wa Vyama vya siasa mara moja kwa mwaka. Washiriki watakuwa ni viongozi watano katika kada ya juu kabisa ya uongozi wa chama kutoka katika kila moja ya nchi 12 za kanda ya ESAURP. Kwa kila nchi, mwanasiasa mmoja atatoka kwenye chama tawala, mwingine kutoka upinzani rasmi, na wengine watatu watatoka katika vyama vya upinzani vilivyobaki. Washiriki wengine katika kikao ni pamoja na wajumbe wa Baraza la Demokrasia na wageni waalikwa kutoka Taasisi za elimu na vyama vya hiari.

i) **Madhumuni ya Kikao**

a. Kuimarisha ushirikiano miongoni mwa vyama vya siasa katika kanda kwa njia ya mijadala kuhusu masuala ya kikanda na ya kimataifa yanayovihusu.

b. Kutunza maelewano baina ya vyama vya siasa kwa kutumia vikao vya pamoja ili kujenga tabia ya kuheshimiana na ustahimilivu wa kisiasa.

c. Kuwawezesha viongozi wa vyama vya siasa kukutana na kukabili masuala yanayojitokeza ya demokrasia na utawala mzuri na kutoa msimamo wa pamoja pale inapowezekana.

d. Kufanya kazi ya kutathmini mradi wa elimu ya demokrasia katika kanda.

ii) **Matokeo**

a. Utamaduni wa demokrasia unaoelekeza kwenye kustahimiliana kisiasa na kuheshimu mawazo ya wengine baina ya vyama vya siasa vinavyotawala na vya upinzani katika nchi wanachama wa ESAURP.

b. Kukuza dhamira ya ushirikiano wa kikanda.

c. Msimamo wa pamoja katika utekelezaji wa maazimio ya msingi na mapendekezo yaliyotolewa na vyama kutoka nchi wanachama.

### 1.3.3 Ufuatiliaji wa Uchaguzi

Hata katika hali ambayo kuna wapiga kura wanaofahamika kikamilifu kidemokrasia na vyama vya siasa imara na vyenye ushindani, nguzo ambayo mfumo wa demokrasia ya kweli inategemea ni utaratibu wa uchaguzi ulio huru na wa haki. Kwa ufupi "demokrasia" ambayo haki binafsi ya mpiga kura, kufanya chaguzi huru za kisiasa inapuuzwa au kuhujumiwa au ambayo vyama vya upinzani vinanyimwa fursa ya kufanya shughuli zao muhimu siyo demokrasia hata kidogo.

Kwa hiyo dhima ya msingi ya ufuatiliaji wa uchaguzi ni kuhakikisha haki na usawa kwa watu wanaoshiriki na vyama vinavyohusika katika uchaguzi. Mpango wa ufuatiliaji uliotajwa hapa ni wa kikanda na utakuwa unajumuisha wafuatiliaji wa uchaguzi waliopata mafunzo kutoka kila moja ya nchi 12 za kanda ya ESAURP.

Ni mawazo yetu kwamba ili demokrasia katika Afrika iweze kutekelezwa kwa namna inayofaa na kupatikana na kuheshimiwa, nchi za Afrika lazima ziweke mifumo yao imara na ya kuaminika ya ufuatiliaji wa taratibu za uchaguzi.

Matukio ya karibuni ya ushuhudiaji wa kimataifa wa uchaguzi yanadhihirisha bayana haja ya ufuatiliaji wa uchaguzi. Ukweli kwamba kazi nyingi katika eneo hili hivi sasa zinafanywa na vyombo kutoka nje ya Afrika kunadhoofisha uaminifu wa jamii ya Afrika. Sasa hivi katika kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika kuna raslimali, ujuzi na utashi wa kisiasa kuunda timu za kanda zinazoaminika za kufuatilia na kutathmini chaguzi kwa gharama nafuu. Zaidi ya hayo washuhudiaji wa kimataifa kama unavyofanywa sasa una kasoro nyingi ambazo zote zinaweza kuepukwa kwa kuunda timu za kikanda za ushuhudiaji.

Hoja zifuatazo zilifikiriwa katika kubuni scheumu hii ya mpango:

a) Ufuatiliaji unaofaa wa uchaguzi unahitaji ushuhudiaji wa kila hatua za taratibu za uchaguzi. Uhaba wa fedha na ugumu wa usafiri na malazi katika siku zilizopita vimeelekea kulazimisha washuhudiaji wa kimataifa kutoka nje ya Afrika kushuhudia upigaji kura peke yake. Kwa kufanya hivyo wameshindwa kutathmini vigezo muhimu vya uchaguzi wa haki, wilaya za uchaguzi na vituo vya uchaguzi, usambazaji wa vifaa vya uchaguzi, nafasi sawa katika kutumia vyombo vya habari na kadhalika.

   Mpango wa ufuatiliaji wa kanda utaweza kutoa tathmini ya uchaguzi iliyo kamili na inayoeleweka kwa sababu matatizo ya mawasiliano ni machache kuliko yale yaliyowakabili washuhudiaji kutoka nje ya kanda.

b) Ushuhudiaji wa kimataifa wa uchaguzi unategemea utashi wa serikali ya nchi mwenyeji. Waangalizi sharti waalikwe kushiriki kwa vile hawana dhamana hiyo kikatiba. Hata hivyo mpango wa kanda wa ufuatiliaji utapaswa kuwa na uhalali wake. Kwa hiyo utakuwa na haki kamili ya kushuhudia chaguzi zote katika nchi zote kumi na mbili zinazoshiriki.

c) Kumekuwa na matukio kadha ambapo wafuatiliaji wa uchaguzi wa kimataifa kutoka nje ya Afrika wamejaribu kuwa kama wasimamizi wa uchaguzi badala ya kushikilia wajibu wao hasa wa kushuhudia na kutathmini uchaguzi. Tatizo hili haliwezi kutokea kwa timu za wafuatiliaji zinazoundwa na wajumbe kutoka katika kanda na kufanya kazi kwa kufuata miongozo fafanuliwa bayana na kukubaliwa kabla.

d) Uamuzi wa nini hasa kinafanya "uchaguzi huru na wa haki" sharti utilie maanani hali halisi ilivyo katika kanda ya ESAURP. Vigezo na kanuni za kutumika katika kutathmini shughuli za uchaguzi lazima vikubalike awali.

i) **Washiriki**

   Viongozi wakuu wa vyama visivyofungamana na upande wowote wanatakiwa wateuliwe na Baraza la Demokrasia ili wawe wajumbe kwenye timu ya usimamizi.

   Zaidi ya hayo, Baraza linaweza kushirikisha wajumbe, kwa mfano msomi ambaye

amebobea katika siasa na wajumbe wengine wa kualikwa kutoka ndani au nje ya kanda. Hii ni moja kati ya maeneo ya mpango huu ambayo yanaweza kunufaika sana kutokana na ushirikiano na wakala wengine.

ii) **Malengo Yalizingatiwa katika Maeneo Yafuatayo:**

a) Makubaliano katika ngazi ya kanda kuhusu ni kitu gani kinajenga "uchaguzi huru na wa haki" na kwa jinsi gani haki itapimwa.

b) Kutoa katika kanda idhini mwafaka na halali ya kuangalia uchaguzi katika kanda ya ESAURP.

c) Kuunda katika kanda kigezo mwafaka na mwongozo wa kusimamia na kutathmini chaguzi ambacho kitatumika kote katika kanda nzima.

iii) **Matarajio**

a) Chaguzi za kuaminika zilizo huru na za haki katika kanda ya ESAURP.

b) Uimarishaji wa kikanda na kukubali kuwepo kwa haja ya chaguzi huru na za haki ndani ya mfumo wa kidemokrasia.

c) Makubaliano ya kikanda na kukubali kuwepo kwa haja ya chaguzi huru na za haki ndani ya mfumo wa kidemokrasia.

Kutoka Gaborone, orodha ya hatua za kufanya iliwekwa ili kuendeleza malengo haya wakati wa chaguzi za madiwani na za Kitaifa nchini Tanzania. Hatua hizo ni pamoja na: kuanzishwa kwa mpango wa elimu ya wapiga kura; semina ya wakufunzi ya kitaifa; semina za wilaya 24 na semina 8 za mashirika yasiyo ya kiserikali.

Semina hizo zilifanyika kati ya Agosti 1994 na January 1995 na zikiweka hatua sahihi ya kujenga hali kamilifu ya kuelewa ya athari za demokrasia ya vyama vingi.

## 1.4 Mpango wa Elimu ya Uchaguzi Tanzania

Mada ambayo ilielekeza michango ya wazungumzaji wote wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Elimu ya Uchaguzi ilikuwa ile isemayo, ili demokrasia ya vyama vingi kufanikiwa, utamaduni wa kidemokrasia na kisiasa unahitajika uundwe kwa kupitia Elimu ya uchaguzi na taratibu za kidemokrasia.

Washiriki 142 ambao walikutana Hotel ya Kilimanjaro, Dar-es-Salaam, asubuhi tarehe 27 agosti 1994, waliwakilisha watoa maoni wa aina mbalimbali katika jamii ya Watanzania. Pamoja na wabunge 41 na madiwani 18, kulikuwepo na wawakilishi 14 wa vyama 10 vya

siasa, waandishi wa habari 28 kutoka vyombo vyote vya habari, washiriki 14 kutoka vyuo vikuu, vyuo, shule na vyama vingine, wawakilishi wa mabalozi na wanataaluma waongoza mjadala 6.

Mpango ulianzishwa kwa kuzingatia kuwa walikuwepo watu ambao sio tu wamejitenga na uchaguzi na kutotumia haki zao za kidemokrasia bali pia hawazijui. Mpango wa Elimu ya Uchaguzi haukuwa ndio mwisho wa tatizo bali njia ya kufikia mwisho wa tatizo. Mwisho wa tatizo maana yake ni watu wapewe uwezo wa kutumia haki zao, kuchagua wanachotaka na kushiriki kwenye utawala wao.

Mradi wa Elimu ya Demokrasia ambao sehemu yake moja ni Mpango wa Elimu ya Uchaguzi una malengo matano: Kwanza, kupatikana kwa wapiga kura katika nchi mbalimbali za kanda ambao wanaelewa haki na wajibu wao. Pili, kwa kuongeza uwezo wa utambuzi, lengo la kuongeza kiwango cha kushiriki katika kupiga kura na kuimarisha demokrasia litafikiwa. Tatu, mradi unakusudia kupata makundi yenye utofauti katika zoezi la kidemokrasia. Nne, kwa kupitia Serikali imara ya kidemokrasia, kutajengeka mazingira ya kisiasa ambayo ni mazuri kwa maendeleo ya kiuchumi. Tano, mpango unalenga kwenye kupata na kushughulikia maoni ya wapiga kura. Mipango mitatu imeanzishwa ili kufikia malengo haya: Mpango wa kwanza ni Mafunzo ya Walimu wa Elimu ya Uchaguzi, Mpango wa pili ni uimarishaji wa uwezo wa usimamizi wa vyama vya siasa, na wa tatu ni ufuatiliaji wa uchaguzi.

Wazungumzaji waliowakilisha serikali zao na vyama vipya walielezea umuhimu wa elimu ya uchaguzi isiyofungamana na upande wowote. Wamesisitiza kuwa badiliko lolote linalotokea katika jamii lazima liwe na manufaa kwa haja za jamii na lieleweke kwao kama linataka liwe na maana. Vyama vya upinzani viliona kuwa Serikali ya chama kimoja imeshika mizizi sana kiasi kwamba imekuwa vigumu kwa watu wengi kufikiria namna tofauti. Hata hivyo, kwa vile sasa imekubalika kuwa maendeleo ya kweli yanahitaji demokrasia ya vyama vingi, ilikuwa ni muhimu kuwa wapiga kura waelimishwe sio tu jinsi ya kuandika kwenye karatasi ya kura lakini pia kuhusu haki zao kama raia. Umuhimu wa kukuza utamaduni mpya wa siasa ambao unaweza kuzuia kutoelewana katika jamii ambako kulikuwa kunabomoa nchi nyingi kulisisitizwa sana. Ndani ya utamaduni huu mpya wa siasa, watu wanaweza kuwa na hakika kuwa chama kilichopo madarakani ambacho hakikuweza "kuzaa matunda" kinaweza kikatolewa.

Haja ya kuwa na elimu ya uchaguzi baada ya miaka karibu 30 ya utawala wa chama kimoja inaonyesha kuwa baadhi ya watu waliofikiria kuwa uteuzi wa wagombea wa CCM kabla ya uchaguzi wa madiwani wa 1994 ulikuwa ndio uchaguzi hasa, walihitimisha kuwa kujiandikisha kwao kama wapiga kura lilikuwa zoezi lisilo na manufaa. Ili kufikia haja hii, mkazo uliwekwa kwenye umuhimu wa kuwepo kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na mradi wa Elimu ya Demokrasia kufanya vizuri. Demokrasia isingeweza kuagizwa, lakini lazima ikue kutoka ndani ya nchi. Kwa hiyo kulikuwa na haja kubwa ya elimu ya uchaguzi.

Mpango uliojadiliwa hapo juu utasaidia vyama vya siasa kama Mmuya na Chaligha katika kitabu chao Towards Multiparty Politics in Tanzania 1992 waliona kuwa ni sahihi:

> Upinzani imara unaweza kupatikana kutoka chama cha siasa au muungano wa vyama vya siasa ambavyo vina uwezo wa ndani wa kuonekana na mpango unaoeleweka; chama ambacho kina upana wa kimipango na uwezo wa kuingiza wanachama wengi; chama ambacho kina malengo mazuri na ambayo yatatumiwa na viongozi na wanachama kama masuala ya kuungwa mkono; chama ambacho kina rasilimali za kutosha hasa wafanyakazi wa kuendesha kazi za chama, na mwisho chama ambacho kinaheshimiwa na kinakubalika katika jamii nzima.

### 1.4.1 Semina ya Kitaifa ya Walimu wa Walimu wa Elimu ya Uchaguzi

Semina hii ilifanyika Chuo cha Ualimu cha Dar-es-Salaam, na ilileta pamoja zaidi ya washiriki 70, hasa kutoka Dar-es-Salaam na Morogoro, ijapokuwa baadhi yao walisafiri kutoka mbali kama vile Arusha na Uingereza. Wote walikuwa watu waliokuwa na nafasi fulani katika Mpango wa Elimu ya Uchaguzi na wengi wao walikuwa washirikishwe katika kuwafundisha wale ambao watakuwa walimu wa kuwafundisha wapiga kura katika zoezi la kupiga kura.

Lengo la semina hii lilikuwa ni kuwaelimisha washiriki kuhusu sheria na Taasisi za mfumo wa uchaguzi chini ya mfumo wa vyama vingi na katika elimu ya wapiga kura. Ili kukidhi haja ya lengo la kwanza, kijitabu kilitolewa na washiriki walielezwa jinsi ya kukitumia katika kutoa Elimu ya Uchaguzi.

Mkutano ulisisitiza umuhimu wa uchaguzi huru na wa haki ambao ulihitaji watu kuelewa na kukubaliana maana yake. Nafasi muhimu ya wanawake ilisisitizwa na semina ilielezwa kuwa ilikuwa ya kihistoria. Kwa ufahamu wake, Waziri wa sheria na masuala ya Katiba, Mheshimiwa S. Sitta, alisema kuwa ilikuwa ni mara ya kwanza zoezi la demokrasia limechukuliwa kwa dhati kiasi cha kufikiria kuanzishwa mpango wa mafunzo kwa wapiga kura. Hali hii itawezesha Watanzania kuwa macho zaidi na haki zao, uchaguzi wa kipi ni kipi, uhuru na wajibu.

Kuundwa na kudumisha utawala wa kidemokrasia kulikuwa ni muhimu sana kwa malengo ya Taifa ya kuchukua kila njia kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na wakati huo huo kudumisha jamii yenye amani.

Nchi ilikuwa sasa kwenye hatua muhimu ya mpito kuelekea kwenye demokrasia ya vyama vingi: baadhi ya chaguzi za vyama vingi zimefanyika, uchaguzi wa serikali za mitaa utafanyika hivi karibuni na uchaguzi mkuu utafanyika mwaka ujao. Matokeo yake kutakuwa hakuna muda wa kutosha wa kuendesha semina za aina hii.

Mwanzoni mwa kitabu, kulikuwa na mada maalumu kama vile Demokrasia na Haki za Binadamu. Nguzo kuu 6 za demokrasia zilikuwa muhimu kama utamaduni wa uhuru wa kidemokrasia unatakiwa uwepo. Nguzo ya kwanza ilikuwa kwamba katiba sio tu

iheshimiwe lakini iwe mali ya watu ambao wataiona kama yao. Pili, lazima kuwe na mgawanyo wa madaraka ili kuhakikisha kudhibitiana katika utekelezaji wa katiba. Tatu, lazima kuwe na kanuni ya sheria ambayo itatumika kwa mapana yake katika nchi na pia kwa ufinyu wake. Nne, kanuni za msingi za haki za binadamu lazima zilindwe. Tano, watu wawe huru kueleza mawazo tofauti ya kisiasa wazi wazi kwa kupitia vyama tofauti vya siasa. Sita, vyombo vya habari visibanwe katika kuelezea na kutekeleza demokrasia.

Ilikuwa ni haki ya mpiga kura kuelimishwa katika misingi na utaratibu wa kupiga kura wa mfumo wa vyama vingi na kuweza kujifunza mipango na sera za kila chama cha siasa na mgombea. Hata hivyo, haki hizi ziambatane na wajibu. Aina mbili kuu za wajibu ni kujua na kufuata sheria za uchaguzi na kupiga kura kama wajibu na bila hofu ikizingatiwa kuwa katika mfumo wa vyama vingi, ilikuwa jambo bora kutofautisha kati ya chama na serikali kwa utaratibu ambao usingeweza kufanyika katika serikali ya chama kimoja: Chama kinaweza kuunda serikali lakini kikabaki na uhai wake wa kipekee. Kwa hali hiyo, taasisi za kitaifa lazima ziendeshwe kwa usawa na bila kuegemea siasa fulani. Vyama vyote vya kisiasa lazima viwe na nafasi katika vyombo vya habari ambavyo inatakiwa isifanyiwe ukiritimba na chama cha serikali. Vilevile, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ionekane kuwa haiegemei siasa fulani.

### 1.4.1.1 Mjengo Mpana: Utendaji wa Mifumo ya Vyama Vingi vya Siasa

Mfumo wa vyama vingi hufanya kazi na hukazia umuhimu wa kutenganisha madaraka kati ya viongozi waliochaguliwa na maafisa tawala. Kundi la kwanza likiwa na wajibu wa kuweka mikakati na kundi la pili likiwa la utekelezaji. Wajibu wa upinzani ni zaidi ya ule wa kusubiri kuingia madarakani, kazi yao ni pamoja na kutia kishawishi na kutoa ukosoaji wa kujenga. Serikali ya wabunge wengi, au ya mseto ya chama chenye wabunge wachache, serikali zote zinaweza kuwa imara ili mradi upinzani una uwezo wa kufanya kazi katika hali ya kujenga na kushawishi.

Vyama vya siasa mara nyingi vimekuwa ni muungano wa haja zisizofanana badala ya kuwa vyama vyenye itikadi moja. Lazima viwe vya kidemokrasia ndani yake vyenyewe na kwamba udikteta ndani ya chama hauna manufaa yoyote kama usivyokuwa na manufaa udikteta nchini. Vyama vina wajibu mkubwa katika zoezi la uchaguzi. Vinahitaji kusaidia na kushiriki katika zoezi la kuandikisha wapiga kura. Kwani kushindwa kupata msaada wao katika zoezi la kujiandikisha kunaweza kukasababisha kushindwa kwa chama katika uchaguzi.

Upangaji wa kampeni na kuziendesha kabla ya uchaguzi ulikuwa muhimu. Utaratibu wa uteuzi na kujitangaza kabla ya siku ya kupiga kura na wajibu wa wafanyakazi wa chama kama wachunguzi wa hatua mbalimbali za zoezi la uchaguzi ni jambo muhimu sana. Kushiriki kwa vyama ni ukaguzi juu ya matendo ya rushwa na kutasaidia kupata haki.

Watu walipigia kura masuala, sera, au watu japo hii ilitofautiana kutokana na haiba ya mgombea mwenyewe au kiwango cha upigaji kura. Hii haikuwa na maana kuwa

hakukuwa na masuala ambayo hayakushindaniwa vikali ambapo vivyo ilikuwa ni muhimu kwamba upinzani ukubali kuwa maoni ya wengi yaheshimiwe. Kuutenganisha utawala kulikuwa ni kizuizi kikubwa dhidi ya rushwa lakini kizuizi kikubwa zaidi kilikuwa ni kutambua kuwa wengi wa wala rushwa hawakuchaguliwa tena.

### 1.4.1.2 Zoezi la Uchaguzi - Sheria na Taasisi

Sheria imeundwa chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa, na inahitaji sio kuibadili kabisa bali kuirekebisha ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa. Sheria ya uchaguzi inashughulikia mambo yote ya uchaguzi. Wagombea walihitajika kuteuliwa kihalali, hii ilimaanisha kuwa wateuliwe na vyama vya siasa vilivyoandikishwa. Madai yoyote ya rushwa, udanganyifu katika uchaguzi yatashughulikiwa na Mahakama Kuu. Utekelezaji mzima wa uchaguzi utasimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo mwenyekiti wake atateuliwa na Rais.

Ilikuwa ni wajibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kukataa shinikizo kutoka kwenye chama chochote cha siasa na kuzuia chama tawala kupuuza matakwa ya kundi lolote. Itakuwa sio jambo la maana, kwa vyama vya siasa kulalamikia Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa matatizo yoyote. Wanatakiwa kuishinikiza serikali kuona kuwa Tume inafanya kazi vizuri. Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa iangalie kwa mapana yake na kurekebisha sheria za uchaguzi ili kuhakikisha kuwa sio tu Tume huru na yenye haki bali inaonekana kuwa ni Tume huru na yenye haki.

Uongozi wa uchaguzi unatakiwa usisitize kuwa utaratibu unaofaa unatokana na haki za mpiga kura na unakuwepo huwa ni njia ambayo watu wanaweza kutumia haki zao za kikatiba kupiga kura kwa uhuru. Mgao wa majimbo ya uchaguzi unaoonyesha kwa mifano kuwa mtawanyo ule ule wa uungaji mkono wa chama unaweza ukatoa matokeo ya uchaguzi tofauti ya jimbo la uchaguzi. Hali hii imesisitiza haja ya kuunda mipaka ya majimbo ya uchaguzi yasiyofungamana na kikundi chochote na kwa serikali kuheshimu mipaka hiyo baada ya kuwekwa.

### 1.4.2 Semina za Mafunzo Wilayani

Semina za Wilaya za Wakufunzi zilifanyika katika wilaya 24 Tanzania Bara (Angalia Kiambatisho A). Mafunzo hayakufanyika Zanzibar kwa sababu Zanzibar ilikuwa haifanyi uchaguzi wa madiwani mwezi Oktoba 1994. Semina hizo zilifanyika katika makao makuu ya wilaya. Washiriki walipeana uzoefu wao wa kuelewa maadili, chama na mazingira ya msingi ya kujengea demokrasia hasa wakati wa mpito kuelekea kwenye demokrasia ya vyama vingi kutoka mfumo wa chama kimoja cha siasa. Mada zilizofundishwa kwenye semina zilikuwa: Tafsiri na Maumbo ya msingi ya Demokrasia; Haki za Binadamu na Uhuru; Mifumo ya siasa ya kutokuwa na chama, chama kimoja au vyama vingi; Vyama vya siasa na Vyama vya Umma; Maana na kazi za mambo yafuatayo katika uchaguzi: Tume ya Taifa ya uchaguzi, waangalizi wa Uchaguzi na wafuatiliaji

uchaguzi; Dola (Bunge, Utawala na Mahakama); Vyama vya siasa; wapiga kura; wagombea uchaguzi; Sababu za uchaguzi; Hatua za zoezi la uchaguzi; Haki na Majukumu ya wapiga kura katika demokrasia ya vyama vingi; Sheria za Uchaguzi; Uandikishaji wa wapiga kura na taratibu za kupiga kura; Njia na nyenzo za kuhakikisha uchaguzi Huru na wa Haki na uhusiano kati ya mfumo wa vyama vingi na maendeleo ya kiuchumi.

Lengo la semina lilikuwa ni kuwafunza washiriki, hasa waratibu wa elimu wa kata, ambao watafanya kazi kama walimu wa viongozi wa maoni katika ngazi ya kata/kijiji. Viongozi wa maoni watafundishwa juu ya haki na wajibu wa mpiga kura na kuhusu uandikishaji na taratibu za uchaguzi. Viongozi wa maoni wanatarajiwa kuwashawishi wapiga kura kwenda kujiandikisha na baadaye kupiga kura. Semina zote zilikuwa za kina na zilikusudiwa kuchukua siku moja nzima ili kupunguza gharama, kwa kuzingatia kuwa katika vituo vingine washiriki wanalazimika kukaa siku tatu nje ya vituo vyao.

### 1.4.2.1 Lengo la Mafunzo

a) Kufunza wakufunzi na viongozi wa maoni ambao watafanya kazi kama walimu na washawishi wa wapiga kura.

b) Kuamsha utambuzi mkubwa miongoni mwa wapiga kura juu ya wajibu wao katika zoezi la kidemokrasia ambapo kutaleta ongezeko katika kushiriki kwao katika kupiga kura na mshikamano wa kudumu wa demokrasia.

c) Kuhimiza kushiriki kikamilifu kwa wanawake kama wakufunzi au wanafunzi ili kuwashawishi kugombea viti vya uchaguzi.

Kama ilivyotajwa awali, wilaya zote 24 zilimalizika ambapo ni kiasi cha robo ya wilaya zote Tanzania Bara. Uteuzi wa wilaya hizo ulitegemea idadi ya kata ambazo zilikuwa na vyama tofauti vya siasa vinavyoshindana katika uchaguzi wa madiwani. Kadhalika, kwa sababu za kiutafiti, wilaya zilizoguswa ni za maeneo ya vijijini, mjini, kilimo, ufugaji na uvuvi.

### 1.4.2.2 Mbinu

Semina ziliruhusu kushiriki kikamilifu (kujifunza kwa kushiriki) kwa wanafunzi. Mihadhara mifupi ilifuatiwa na kipindi cha maswali na majibu. Maswali kutoka kwa wanafunzi yalitegemewa yasaidie kujifunza zaidi masuala na mara kwa mara kukosoa kile walichokiona kuwa ni kibaya katika mfumo. Maswali kutoka kwa wakufunzi yalikusudiwa kugundua kama wanafunzi wamezingatia vizuri masuala na kama walikuwa wanaweza kuelezea maswala kwa viongozi wa maoni. Kijitabu na vitini maalum vilikuwa ndio silaha kuu katika majadiliano katika semina.

### 1.4.2.3 Idadi Iliyopata Mafunzo

Mafunzo katika ngazi ya wilaya yaliwafikia wanafunzi 685. Kati ya hao, wanafunzi 350

walikuwa wanaume na 335 wanawake. Maelekezo yalikuwa idadi ya wanafunzi (waratibu wa elimu wa kata) iwe nusu wanaume na nusu wanawake. Katika wilaya ambazo zilikuwa na waratibu wa elimu wanawake wachache, walimu wakuu wanawake au walimu wanawake walialikwa kuwa wanafunzi. Hata hivyo, jedwali katika kiambatisho A linaonyesha kuwa Moshi vijijini viongozi hawakufuata maelekezo.

Waratibu hawa wa elimu wa kata 685 walikuwa wafundishe viongozi wa maoni 97,757. Viongozi wa maoni ni watu wanaofahamika ambao wanaweza kuwashawishi wengine kwenda kujiandikisha na baadaye kupiga kura. Mara nyingi hawa watakuwa walimu wa shule za msingi, wafanyakazi wa vyama vya ushirika, vijana na viongozi wanawake, viongozi wa dini, wazee, wafanyakazi wanaojulikana na wafanya biashara. Viongozi wa maoni baadaye wanatakiwa nao kuhamasisha wapiga kura wapatao milioni 2.5. Kila kiongozi wa maoni alitegemewa kuhamasisha wapiga kura walengwa 20 kwa kiwango cha chini.

Kati ya vijitabu 700,030 vilivyochapishwa, 692,000 vilisambazwa. Kwa upande wa vijitabu vilivyobaki, baadhi vilitumika kwenye mafunzo ya ngazi ya Taifa na baadhi vilitumiwa na semina maalumu za mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) zilizofanyika mwezi Desemba kwa msaada wa NOVIB. Vijitabu vingine vilitumika kuwafundishia wafanyakazi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) mwezi Januari 1995. Kwa ujumla dodoso 3,525 zilikusanywa kutoka kwa wakufunzi na vingozi wa maoni.

### 1.4.3 Semina za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs)

Mwezi Desemba 1994 wakufunzi wa ESAURP walitoa semina katika vituo 7 nchi nzima (pamoja na Zanzibar) kwa wafanyakazi wa mashirika yasiyo ya Kiserikali. Kwa pamoja washiriki 611 walihudhuria semina. Mbali na kuwafundisha masuala yanayohusiana na mpito wa kuelekea kwenye demokrasia ya vyama vingi, sababu nyingine ya semina ilikuwa ni kuanzisha kiungo kati ya ESAURP na Mashirika yasiyo ya kiserikali katika uchaguzi wa mwaka 1995.

Kinyume cha matarajio ya wakufunzi wengi, washiriki wa semina za Mashirika yasiyo ya kiserikali walionekana kuelewa kwa undani na kuweza kuchambua maswala ya kisiasa vizuri ukilinganisha na semina nyingine zilizopita zilizowahusisha waratibu wa elimu wa kata. Idadi kubwa ya washiriki wa Mashirika yasiyo ya kiserikali walikuwa watu ambao walikuwa ama kwenye siasa (viongozi wa vyama vya siasa, jumuiya za chama cha siasa) na watumishi wa serikali waliostaafu ambao walitaka kujiweka sambamba na wakati kwa kufanya kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Mchanganyiko huo ulileta majadiliano hai ambayo yalisaidia kubadilishana maarifa na uzoefu. Hata hivyo katika vituo fulani kulikuwa na wakati kulitokea majadiliano makali kwa vile washiriki waliendelea kujitambulisha na vyama vyao vya siasa.

Hali hii ilitoa mtihani mkubwa kwa mwenyekiti ambaye alitakiwa atulize hasira za washiriki kwa kusisitiza sifa ya uvumilivu na kuheshimu mawazo ya wengine hasa katika mfumo wa vyama vingi.

### 1.4.4 Maoni ya Washiriki wa Semina

Maoni yafuatayo yalitolewa na wanasemina katika ngazi ya Taifa na Wilaya na pia washiriki wa semina za mashirika yasiyo ya kiserikali.

1. Wanasemina waliulizia umuhimu wa katiba ya Tanzania chini ya demokrasia ya vyama vingi. Walifikiri kwamba ni vyema vyama vya siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali, makundi ya kitaalamu, makundi maalumu na watu binafsi wafanye mkutano wa katiba na kujadiliana juu ya katiba inayokubalika. Wamekosoa utaratibu unaoendelea wa kuiweka viraka katiba ya sasa.

2. Wasiwasi ulitolewa wa ukosekanaji wa maandishi kuhusu sera za vyama vya siasa. Walidai kuwa kukosekana kwa maandishi haya kulisababisha wapiga kura kushindwa kutoa uamuzi wa kufaa kuhusiana na sera bora ya chama.

3. Tume ya uchaguzi ya Taifa ifahamishe mapema taratibu za kupiga kura ili wapiga kura wajue mapema wanatakiwa kufanya nini kabla ya uchaguzi mkuu.

4. Washiriki wa semina walibaini kuwa pamoja na semina za mafunzo kwa wapiga kura ni vema pawepo pia semina kwa viongozi wa vyama vya siasa ili kuelimisha utamaduni wa kidemokrasia na kisiasa chini ya mfumo wa vyama vingi.

5. Ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki ilishauriwa kuwa vyama vyote vya siasa vilivyoandikishwa viwe na nafasi sawa katika vyombo vya habari na ruzuku ya fedha ya Serikali.

6. Kwa kuzingatia uchaguzi mdogo wa Kigoma ambapo mgombea asiye Mtanzania alichaguliwa kuwa mbunge na kwa kuzingatia idadi kubwa ya wakimbizi kutoka Rwanda wanaoingia Mkoa wa Kagera, washiriki walifikiri kwamba vyombo vya serikali lazima viwe macho wakati wa uandikishaji wa wapiga kura ili wale ambao sio Watanzania wasipewe nafasi ya kushiriki kama wagombea au wapiga kura.

7. Washiriki walishauri kuwa karatasi za kura zihesabiwe kwenye kituo cha kupigia kura kila inapowezekana ili kupunguza udanganyifu ambao unaweza kutokea wakati wa kuhamisha masanduku kwenda kwenye vituo vya kuhesabia kura.

8. Washiriki walishauri kuwa, Tume ya Uchaguzi Taifa iwe huru na kama inawezekana iwe na wawakilishi kutoka kwenye vyama vya upinzani. Kwa kufanya hivyo, hii itasaidia kupunguza malalamiko ya hivi karibuni ya maamuzi yake kadhaa.

9. Washiriki walionyesha wasiwasi wao kuhusu kutokuwepo kwa maafisa wa Tume katika ngazi ya mkoa na Wilaya na hivyo kuwafanya watumishi wa serikali kufanya kazi kwa niaba yao. Maafisa utawala hawa wa mkoa na wilaya sehemu nyingine wamefanya kazi kwa kukipendelea chama tawala.

10. Washiriki walipendekeza kuwepo na orodha ya kitaifa ya wapiga kura ambayo inaweza kurekebishwa upya baina ya chaguzi. Maafisa wa uchaguzi wangeweza kufanya utafiti na kurekebisha orodha hiyo kila inapotakiwa kwa kufuta waliokufa na kuongeza wanaofikia umri wa miaka 18. Hali hii itapunguza kususia uchaguzi.

11. Magazeti na redio yalipendekezwa kama taasisi muhimu za kufanya kazi za ESAURP zijulikane. Kwa hiyo mpango wa elimu ya wapiga kura ni vema utayarishwe na ESAURP kwa ajili ya wafanyakazi wa vyombo vya habari.

12. Mashirika yote yasiyo ya kiserikali (NGOs) yameomba yawe ama vituo vya mpango wa elimu ya wapiga kura au washiriki katika mpango wa mafunzo. Kutokana na ukosefu wa fedha, mashirika mawili tu yasiyo ya kiserikali yalionyesha nia ya kuchangia mipango ya elimu ya wapiga kura.

SURA 2

# ATHARI ZA MAFUNZO YA SEMINA ZA WALIMU

## 2.1 Athari Kamilifu

Mpango wa mafunzo kwa walimu ni sehemu ya mradi wa Elimu ya Demokrasia. Kuna mipango mingine miwili: uimarishaji wa uwezo wa usimamizi wa chama cha siasa (ambao unajumuisha: mafunzo ya wafanyakazi wa chama, msaada wa utafiti wa uwandani kwa wanafunzi wa uzamili, likizo za kunoa ubongo za kitaaluma na mikutano ya kanda) na usimamizi wa uchaguzi.

Kwa hiyo, kimsingi, kila upimaji ni lazima ufanyike mwishoni mwa miaka mitatu ya mwanzo, wakati ambapo mradi mzima utakuwa uko tayari kufanyiwa tathmini. Mipango hii ya mafunzo ni ya kutoa elimu ya kukuza demokrasia miongoni mwa wanasiasa na kwa umma mzima unaojihusisha na hali bora ya Taifa. Kwa hali hiyo, athari yoyote haiwezi kuonekana mara moja. Hata hivyo, shinikizo la kutaka kujua athari za mafunzo kutoka sehemu mbalimbali ni kubwa kiasi kwamba ni vema kusemea kidogo jambo hilo.

Semina za majaribio za elimu ya kupiga kura zilifanyika katika wilaya 24 kati ya wilaya 104 kabla ya uchaguzi wa madiwani. Matarajio yalikuwa kwamba upigaji kura katika wilaya hizo 24 utaonyesha dalili za athari za mafunzo, yaani, kupata asilimia kubwa ya wapiga kura kuliko wilaya ambazo hazikupata mafunzo ya aina yoyote. Semina zilitarajiwa kupiga vita upuuzaji, kuinua kiwango cha uandikishaji wa wapiga kura na hivyo kupata kiwango kikubwa cha upigaji kura. Lakini, hata katika wilaya hizo 24, mambo mawili yanaweza kusemwa. Ukiondoa Dar es Salaam ambapo uandikishaji uliingiliana na muda wa kutoa semina, katika wilaya 21 zilizobaki, Semina zilifanyika baada ya uandikishaji kufanyika. Pili, matukio kadhaa makubwa yaliathiri kujitokeza kwa watu. Kwa hiyo athari kamilifu ya mafunzo ingeonyesha kupanda kwa asilimia fulani ya wapiga kura wanaostahili wakati wa kujiandikisha na kupiga kura kwa wingi katika wilaya hizo 24 ukilinganisha na wilaya zilizobaki. Wakati kitabu hiki kilipokuwa kinaandikwa, ni takwimu za waliojiandikisha tu ndizo zilizokuwa zimetolewa. Mlinganisho wa namba kuhusu nani amejiandikisha na idadi sahihi ya wale waliopiga kura haikuweza kupatikana.

## 2.2 Matukio Yaliyoingilia Athari

Hata kama takwimu sahihi zingepatikana, tathmini isingekuwa kamilifu kutokana na matukio mengine muhimu ambayo ama yalitokea wakati wa kupiga kura au yalikuwa yanajijenga. Matukio hayo ni yale yanayowagusa sana watu kama vile upungufu wa maji, mgao wa umeme, bili kubwa za simu ambazo hazifanyi kazi, bei kubwa za bidhaa na kodi ya maendeleo. Mwisho wa yote kulikuwa na tatizo la kifedha ambalo lilitokea kwa sababu serikali imeshindwa kuongeza pato la Taifa.

2.2.1 Juhudi za Wizara ya Fedha za kukusanya kodi hazikupata mafanikio. Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri mpya wa Fedha alinukuliwa na gazeti la Daily News la Jumanne, Disemba 13, 1994 kama ifuatavyo:

> Waziri Kikwete, ambaye aliteuliwa kuishika Wizara Jumatano iliyopita na kuapishwa Jumapili, alisema "Tuko nje ya mstari. Utendaji wa serikali haukuwa mzuri katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita".
>
> Akiwa amekaa karibu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Peter Ngumbulu, Waziri alieleza shughuli zinazopewa kipaumbele na wizara, akisema kuwa ni pamoja na kusukuma ukusanyaji wa kodi na kuwaelekeza wote wale wanaodaiwa na serikali kulipa madeni yao haraka.
>
> Waziri aliwaeleza waandishi wa habari kuwa Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa serikali alikuwa bado anachunguza mashirika ambayo yanadaiwa kuwa yamekwepa kulipa kodi au yamepata msamaha wa kodi isivyo halali, na kwamba kampuni nane zinadaiwa na serikali zaidi ya bilioni 4.2.
>
> Kanali Kikwete ameyapa mashirika hayo hadi Disemba 31, kulipa kodi zao. Alizitaja kampuni hizo kuwa ni Merchant Vintners Limited, ambayo inasemekana kuwa imeingiza bia za Stella Artois, ambazo zinadaiwa ushuru wa Shs. 2,995,124,665/=.
>
> Kampuni nyingine ni TRADECO Shs. 987,494,281/=; Biashara Consumers Limited 7,528,538/=; Massawe and Company 47,028,497/=; Factory Agent 96,269,323/=; Metha and Brothers 51,451,592/ = Caltex Oil 6,075,132/=; na Fazal and Company Limited 29,174,058/=.
>
> Kanali Kikwete amesema kuwa ripoti ya awali ya Msimamizi na Mkaguzi Mkuu juu ya Shs. 15,442/ = million za wakwepa kodi, imeonyesha kuwa Shs. 238,696,926/= zimelipwa ambapo kiasi cha Shs. 663,962,442/= zilikuwa zimesamehewa.
>
> Ripoti imeonyesha pia kuwa kodi ya Shs. 1,618,126,091/= ilikuwa haikulipwa kwa kuwa ilihusu mizigo inayopita, ambapo Shs. 5,249,664,710/= ilihusu mizigo iliyoko kwenye mabohari ya dhamana.
>
> Waziri alisema kwamba uchunguzi utafanywa kwenye mashirika mawili yaliyoko Arusha na baadhi ya makampuni ya mafuta ambayo yamesemekana kuwa yanadaiwa na serikali zaidi ya Shs. 3.4 bilioni.
>
> Kanali Kikwete amesema kuwa Wizara yake itatazama upya sera za Taifa za fedha na kujaribu kuangalia sababu za kushindwa kukusanya kodi ipasavyo na katika wakati uliopangwa.
>
> Alisema, "Labda mfumo ni mbaya au kodi ziko juu mno kiasi kwamba zinashawishi ukwepaji".
>
> Waziri aliwaeleza zaidi waandishi wa habari kuwa uhusiano kati ya Tanzania na Jumuiya ya Wafadhili kwa hivi karibuni umekuwa mchungu, na kwamba hali hii imesababishwa na uendeshaji mbaya wa mambo ya fedha, hasa ukusanyaji mdogo wa kodi.
>
> Alikiri kuwa "Wafadhili hawatakuwa na furaha hadi tutakapokusanya kodi kwa bidii. ...Kile watupacho kama msaada ni fedha iliyolipwa na walipa kodi wa nchi zao".
>
> Waziri amesema kuwa anatumaini kuwa wafadhili hivi karibuni watarudisha imani yao kwa Tanzania kwa sababu serikali imejizatiti kutatua matatizo yaliopo.

Takwimu zimetajwa na Mkaguzi Mkuu na kuwa ni za kustaajabisha, lakini tabia ya

kukwepa kodi na misamaha bado ipo. Hata kama takwimu zitakuwa sahihi kiasi gani, ukweli unabaki kuwa maendeleo duni ya kiuchumi yakiambatana na mlipuko wa bei na uzalishaji wa chini ndio masuala muhimu zaidi kwa wananchi kuliko mabadiliko ya Serikali ya mitaa. Bwana Robert MacNamara ambaye aliwahi kuwa Rais wa Benki ya Dunia ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Muungano wa Dunia kwa ajili ya Afrika aliuliza swali la msingi kuhusu jambo hili. Alisema "Je mtu anaweza kukadiria kiasi cha kukata tamaa cha binadamu wakati ambapo pato lao lote lisilotosha linaangukia chini ya kiwango chao cha awali na wakati kuna matumaini machache ya kupata ongezeko la kutosha katika muongo ujao?" (7/15 Draft- Stockholm 7/22/94).

**2.2.2** Suala lingine zito ambalo limekengeua uangalifu wa watu lilikuwa ni kiasi kikubwa cha uhuru wa habari ambao umewaelekeza watu kwenye masuala muhimu zaidi ya kufa na kupona: bei ya kahawa ya wakulima, kupanda kwa kiwango cha uhalifu, ubadhirifu wa fedha za umma, kuanguka kwa vyama vya ushirika, kukosa ajira kwa vijana, maandamano ya wanafunzi, na shinikizo la suala la mazingira mabaya ya kazi kutoka kwenye vyombo vya kitaalamu n.k. Suala la Serikali ya Tanganyika limeleta utatanishi mkubwa katika chama (CCM) na katika Bunge kiasi kwamba kila lililowezekana lilifanywa katika kutafuta ufumbuzi. Kulikuwa na suala la Muungano na swala la Zanzibar kujiunga na Shirika la Nchi za Kiislamu (OIC). Yote haya mawili yalizua maswali kuhusu katiba na uongozi.

**2.2.3** Toleo la The East African la Februari 13-19, 1995 lilikuwa na makala ambayo ilitoa mahojiano kati yake na Rais wa zamani wa Zanzibar Mheshimiwa Aboud Jumbe:

> **Jumbe:** Kitu kinachotakiwa cha haraka sio kura ya maoni, bali kuwa na utaratibu ambao utahakikisha kuwa ukiukwaji wa katiba unaweza kurekebishwa.
>
> **E.A.:** Wanasiasa wengine wanadai mkutano wa Katiba. Je wewe uko kwenye kundi hili?
>
> **Jumbe:** Bado sijalizingatia sana suala hili. Lakini kwa upande wa serikali ya Muungano, jibu liko kwenye kutekeleza makubaliano ya mwaka 1964 na kufanya marekebisho kwa kutumia njia sahihi.
>
> **E.A.:** Je ungependa kuundwa upya kwa serikali ya Tanganyika?
>
> **Jumbe:** Hakuna shaka kuwa serikali ya Tanganyika iliondolewa bila sababu yoyote, pasipo haki na kwa msingi isiyo ya kikatiba. Watanganyika wana haki ya kuidai.

**2.2.4** Kitabu cha Mwalimu Nyerere cha 1994 (**Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania:**) kiliitikisa nchi na tangu kuchapishwa kwake kumekuwa na matukio kadhaa muhimu na mashauriano yenye athari kubwa kiasi kwamba Rais Mwinyi alilazimika kulivunja baraza lake la mawaziri akiwa Dodoma, Desemba 1994 na kumlazimu Horace Kolimba, Katibu Mkuu wa CCM kujiuzulu na Cleopa Msuya kuchukua nafasi ya John Malecela kama Waziri Mkuu na Makamu wa kwanza wa Rais. Gazeti la The East African la Novemba, 7-12, 1994 liliandika kuhusu jambo hili.

> Mwalimu Julius Nyerere katika kitabu ambacho kitawashangaza Watanzania wengi, amedai kuwa maafisa wawili wa ngazi za juu wa serikali na chama tawala wajiuzulu au wafukuzwe.

Kitabu pia kinamlaumu Rais, aliyemfuatia, Ali Hassan Mwinyi kwa kushindwa kuwashughulikia watu hawa wawili - Waziri Mkuu na Makamu wa kwanza wa Rais, John Malecela na Bwana Horace Kolimba, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kinachotawala.

Katika nchi iliyozoea kuwashughulikia viongozi wake wote kwa heshima kubwa, hasa wakati wa utawala wa muda mrefu wa Rais Nyerere mwenyewe, kitabu Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania kinatarajiwa kuwa kitashtua fikra za wananchi wengi.

Kwa maana fulani, Rais mstaafu anawaeleza Watanzania wenzake: "Amkeni, muda umewadia kwenu ninyi kutambua kuwa mnayo haki ya kujieleza".

Lakini ngoja kidogo. Watanzania wengi leo hii wana shauku kidogo sana katika mfumo wa siasa ambao wanaamini unawajibika katika kuunda miungu ambao wanashabikia utajiri wakati wao wenyewe wanaendesha maisha yao kwa taabu. Hata hivyo, wanasema, Nyerere alikuwa mjenzi wa mfumo huu. Kiongozi wa Tanzania kwa zaidi ya miongo miwili, Nyerere mstaafu bado ni kipenzi cha wengi - pamoja na vyombo vya habari - hapa nchini na nje ya nchi; lakini bado ni watu wachache watapendezewa na kitabu chake cha hivi karibuni, ambacho misingi yake imetiliwa mashaka hasa katika maswali yaliyoulizwa na wengi katika mikutano ya waandishi wa habari.

Bwana Kolimba alikataa katakata kujiuzulu siku moja baada ya mwalimu kuzindua kitabu chake. "Watu wataamua," Kolimba aliwaambia waandishi wa habari.

Kwa kweli, Nyerere amemshutumu Malecela na Kolimba kwa kushindwa kulishughulikia vema suala lililokufa la Zanzibar kujiunga na OIC mwaka 1992. Wakati Zanzibar ilipoomba uanachama, Mwalimu anadai kuwa, Malecela na Kolimba walijua vema suala hili. Badala ya kuleta suala la OIC kwenye Kamati Kuu ya chama tawala, Nyerere anasema watu hawa wawili walipeleka mbio suala hili na kumshawishi Rais Mwinyi kulikubali kisiri - hadi lilipojitokeza kama kashfa ya kitaifa kabla hali hiyo pia kupatiwa suluhu.

Nyerere tena anawashikilia Malecela na Kolimba kuwa wanawajibika na matukio mengine yaliyofuata ambayo yalisababisha mwito wa Wabunge 55 wa Tanzania Bara kudai Serikali ya Tanganyika ili kulipiza kosa la Zanzibar la kukiuka Katiba.

Hali hii ya kutoshughulikia vizuri maswala muhimu ya Kitaifa, imemweka Rais Mwinyi mahali pagumu, Nyerere alisema, na kwamba watu hawa wawili ni lazima waondolewe kwenye uongozi.

**2.2.5** Kosa ambalo limefanywa bila kutarajia: Siku chache kabla ya uchaguzi wa madiwani, CCM katika jitihada zake za kutaka kuwa wanademokrasia zaidi walitoa utaratibu wa kuteua wagombea watakaogombea uchaguzi. Kwa jicho la wengi, tayari huu ulikuwa ni uchaguzi wa madiwani. Kuwepo kwa pengo la uongozi, kutokana na CCM kutohitajika tena kuhimiza uchaguzi kwa kuogopa madai kuwa waliwashawishi watu kupata kura, kulifanya uchaguzi wa madiwani kutokuwa na maana.

**2.2.6** Karibu na muda wa uchaguzi wa madiwani, vyama vipya kadhaa vya kisiasa vilikwisha anza kugombana wenyewe kwa wenyewe, kutengana na kuonyesha hali ya kutomudu. Kwa watu wengi vyama hivi vya siasa havikuonekana kuweza kuchukua nafasi za Serikali za mitaa zinazoendeshwa na CCM. Orodha ya matukio yenye athari mbaya kwa Watanzania wengi haiwezi kumalizika.

## 2.3 Apathi*

Mbali na matukio ambayo yanasemekana yameingilia utekelezaji, kiwango apathi katika Tanzania ni cha juu na hili ni bunio la utafiti. Jibu lake lazima litokane na swali linalotaka kujua kwa nini watu hawajiandikishi na wale wanaopiga kura wanapigia kura kitu gani. Matukio haya ni nyongeza kwenye hali ambayo ipo tayari miongoni mwa Watanzania ya kutojali masuala ya Kitaifa.

Kwa mfano, katika uandikishaji wa kwanza wa madiwani katika Dar es Salaam, idadi ya waliojiandikisha ilikuwa watu 169,835 na ikaongezeka hadi watu 175,638 ikiwa ni ongezeko la watu 5,800 katika uandikishaji wa pili ambapo wale wanao stahili kupiga kura katika Wilaya zote tatu za Dar-es-salaam ni 700,000.

Sababu hasa za kuwa na kiwango hiki kidogo cha watu waliojiandikisha zilitolewa: Kwanza, kulikuwa na hali ya kuchanganyikiwa katika fikra za wapiga kura kati ya njia ya zamani ya kupiga kura ya chama kimoja na mahitajio ya upigaji kura mpya wa vyama vingi. Pili, safari hii, viongozi wa CCM wameacha kampeni zao kabambe za kawaida za kuwahimiza wapiga kura kwenda kujiandikisha, wakiogopa kulalamikiwa kwamba wamejichukulia nafasi kubwa mno. Tatu, taasisi ambazo zinafanya kazi kwa ajili ya demokrasia zimepata pigo la kukosa fedha, na hizo zilipopatikana, zilikuwa zimechelewa na chache. Nne, majukumu yaliyotabiriwa yachukuliwe na taasisi mbalimbali katika kuwashawishi wapiga kura wanaostahili yalikuwa hayajulikani vema kuwa ni yapi.

Matokeo haya ya chini ya kujiandikisha yameonyesha kiasi cha apathi cha kupiga kura miongoni mwa wapiga kura, na kwa kiasi kikubwa yanaonyesha haja ya kuwa na elimu ya uraia iliyopangwa vizuri.

Umuhimu wa serikali na chombo chochote kinachopanga uchaguzi wa kuwa na mipango madhubuti hauwezi kupuuzwa. Kwa sababu kama NEC ingepanga mapema uandikishaji wa wapiga kura za udiwani, wasingelazimika kuharakisha zoezi la uandikishaji ambalo matokeo yake lilipata chini ya asilimia 4 kati ya uandikishaji wa kwanza na wa pili katika jiji la Dar es Salaam.

Katika mkutano wa Gaborone, Waziri Chiepe alikuwa na haya ya kusema:

> Zoezi la kidemokrasia linajumuisha kanuni za usawa za haki na nafasi za maisha, kibali kutoka kwa wale wanaoongozwa na kutokuwepo na uchokozi wa kutoka nje. Zoezi la kidemokrasia linakuwa limekamilika ikiwa kila mpiga kura anafahamu haki zake za kidemokrasia za kushiriki katika uchaguzi akijua kuwa kura yake inaweza ikaleta tofauti kubwa. Kwa hali hii, suala la apathi katika kupiga kura lazima lipigwe vita kwa nguvu kama maoni ya watu wote yanatakiwa kupatikana katika kuunda serikali na katika maeneo ya upinzani. Kwa hiyo ni jambo la kushukuru mno kuzingatia kuwa elimu kwa ajili ya kumwezesha mtu afaidi kikamilifu haki zake

---

* Hali ya kukata tamaa, kuvunjika moyo na kutokuwa na matumaini

za demokrasia ni mojawapo ya nguzo kuu za mradi wa elimu ya demokrasia. Serikali yenye ubinadamu, kusikiliza, na imara inaweza kutokea tu kwa kupitia wapiga kura imara na walio macho. Serikali kama hizo zinaweza pia kuchochea na kudumisha ushirikishwaji wa wananchi katika mambo ya umma katika kipindi chote ikiwa madarakani.

## 2.4 Athari Halisi

Kwa hiyo kipimo cha athari lazima kijikite sio kwenye mafikirio tu bali kwa kutumia vionyesheo vya kijamii ambavyo haviwezi kupimwa kwa takwimu. Basi, sehemu iliyobaki ina shughulikia uhakiki juu ya elimu ya wapiga kura katika wilaya 24 za Tanzania Bara. Vionyesheo hivyo ni pamoja na shauku (fungua dimba: angalia maoni ya Ramadhani katika Ripoti ya Elimu ya wapiga kura), matangazo ya vyombo vya habari, kuialika ESAURP kutoa mihadhara kwenye makundi yanayopenda, maombi kwa ESAURP ya kuendesha semina za aina hiyo kwa watu wengine, Serikali ya Zambia, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Walimu wa Walimu wa Chuo cha Ushirika na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs). Zaidi ya vionyesheo vyote hivi, kuna matokeo ambayo yameripotiwa katika sura ya Nne na Tano.

**2.4.1** Kulikuwa na shauku kubwa miongoni mwa waliohudhuria kozi ambao walifika kwa wingi kuliko ilivyokuwa imepangwa. Maswali yaliulizwa kuanzia maswali ya msingi kama vile nini maana ya demokrasia ya vyama vingi na kama inaleta tofauti yoyote. Katika siku za hivi karibuni, maandishi yameshauri kuwa shauku hushinda hofu na vitisho, sifa ambayo ni muhimu miongoni mwa wanyonge na wasio na elimu. Msomi maarufu wa Kiafrika, Ali Mazrui hushabihikia mawazo mapya na kwa upande wake hivi ndivyo msomi anavyotakiwa kuwa.

**2.4.2** Kipimo cha pili cha pembeni cha kupima athari kilitokana na matangazo ya vyombo vya habari katika kipindi cha mafunzo ya semina za wakufunzi. Televisheni, magazeti, redio zilitangaza semina na kutoa maoni.

Kati ya Agosti 26 na Oktoba 15, 1994 kulikuwa na matangazo ya kutosha ya vyombo vya habari kuhusu mpango wa elimu ya kupiga kura. Magazeti yaliyokuwa na makala juu ya mpango huu kabla na baada ya semina yalikuwa: Daily News, Mzalendo, Express, Business Times, Majira, Rai, Kiongozi, Uhuru na Nipashe.

Radio Tanzania ilikuwa na matangazo ya mara kwa mara ya ratiba ya mafunzo na ilitangaza baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yameulizwa katika baadhi ya semina.

Mikutano hii ya waandishi wa habari baadaye ilifuatiwa na matangazo ya redio na magazeti. Kutokana na maswali yaliyoulizwa na waandishi wa habari kwenye mikutano hii na pia kutokana na makala zilizotokea kwenye magazeti, uandishi wa habari unakiri pia kuwa elimu ya kupiga kura ni sehemu muhimu katika ujenzi wa utamaduni wa demokrasia katika Tanzania.

**2.4.3** Kipimo cha tatu juu ya athari kilionekana kutokana na maombi mengi yaliyotaka wajumbe wa Sekretarieti ya Baraza la Demokrasia kutoa mihadhara kwenye semina na mikutano iliyotayarishwa na makundi mengine ndani na nje ya Tanzania: Semina za KKKT huko Moshi, African American Institute huko Victoria Falls Zimbabwe mwezi Novemba 1994, Semina ya NOVIB/CUSO huko Arusha ya mwezi Novemba 1994.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Zambia, Brigedia Jenerali Godfrey Miyanda ameiomba rasmi ESAURP kuendesha semina za walimu wa walimu nchini Zambia mwaka 1995 kabla ya uchaguzi wa madiwani. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania limeandika kuomba rasmi semina za demokrasia kutolewa kwa viongozi wake 100 mwezi Desemba 1994. Vyama viwili vya, CCM na UDP na wabunge wawili waneomba semina hizo. Chuo cha Ushirika Moshi kimeomba kuandaliwe semina kwa ajili ya walimu wake hapo Chuoni na kwa wakufunzi wao wa uandani; na warsha ya siku mbili ilitolewa kwa wawakilishi kutoka mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's) 230 na kiasi cha watu 611 kwa ujumla walishiriki katika vituo 7 wiki moja kabla ya Krismasi ya 1994. Hiki kwa kweli ni kipimo cha 4 muhimu cha kudhihirisha athari njema za semina za walimu wa walimu katika Tanzania.

**2.4.4** Kionyesheo kingine dhahiri cha kupendwa kwa semina za walimu wa walimu ni michango ya fedha iliyotolewa na wafadhili wa ndani na nje. Kipengele cha fedha hakionekani kwa wingi wa fedha taslimu, au thamani kifedha, bali kwa orodha ndefu ambayo imejumuisha hata wafadhili wa kiserikali ambao sio wale wa kawaida. (angalia kiambatisho 2).

Gazeti la Express lilikuwa na makala ifuatayo kati ya Septemba 22-24, 1994.

> "Kazi imekwisha aanza kufanywa kote Tanzania na watafiti wa mpango wa Utafiti wa Vyuo Vikuu vya Mashariki na Kusini mwa Africa (ESAURP) ya kufundisha wakufunzi wa elimu ya kupiga kura.

Mradi wa Elimu ya Demokrasia unafanya kazi na chama cha siasa kilicho madarakani au vyama vya upinzani, kuimarisha demokrasia katika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Hali hii ni ya kuboresha utawala, kuendeleza haki za binadamu, kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kusaidia kuepukana na maafa ya binadamu ya vita na watu kusambaratishwa.

Wakati wa kuandika kuhusu mradi huu. Mkurugenzi mtendaji wa ESAURP alisema kuwa uhalali wa mradi huu unatokana na kule kupunguza hofu miongoni mwa watu katika nchi nyingi za kiafrika ambapo pana ukandamizaji, na ambapo pana mfumo wa chama kimoja, kwamba kuelekea kwenye siasa za vyama vingi kutaambatana na ghasia za kisiasa.

Tukinukuu mfano wa Angola tunaona kwamba UNITA ilikataa kukubali kushindwa uchaguzi na baada ya hapo pakatokea ghasia za kisiasa, tofauti na kule Zambia, ambapo chama kilichokuwa kinatawala kilikabidhi madaraka kwa mshindi na hivyo kukubali sheria za mchezo.

Nchini Malawi, makabidhiano ya madaraka yaliripotiwa kuwa yalikuwa ya pole pole sana.

ESAURP inaamini kuwa jamii za Kiafrika zimewekwa kwenye hali mbaya na isiyo salama na hazina uhakika kama mfumo wa vyama vingi ndio njia bora ya kuendelea nayo.

## 2.5 Mashaka ya Wanasemina Kuhusu Mtaala

Wanasemina walitoa maoni yao kuhusu semina juu ya masuala kadhaa na hivyo bila kukusudia wakawa wanafanya tathmini. Ukiangalia maoni yao kwa undani utapata hisia zao kama ifuatavyo:

### 2.5.1 Demokrasia na Haki za Binadamu

Wanasemina waliisakama Katiba ya Muungano yenye viraka na walidhani kuwa ni bora kama ingefanyiwa marekebisho, ikachapishwa na kisha ikauzwa kwa bei nafuu ili kuwawezesha wapiga kura kuinunua. Wanasemina wengine walidhani kuwa vyombo vya habari vya Tanzania bado vinatakiwa viwe huru zaidi kwa sababu ya kuingiliwa mno na serikali. Ilibainika kuwa wale ambao walikuwa wanakiuka Katiba ya Tanzania waliachiwa huru hasa wanapokuwa viongozi wa Kitaifa.

### 2.5.2 Sheria na Taratibu za Kupiga kura

Wanasemina walitanabahisha juu ya umuhimu wa kusafirisha masanduku ya kura haraka na kwa usalama. Waliona kuwa kazi ya kuhesabu karatasi za kura ingefanyika katika vituo vya kupigia kura.

Maswali yaliulizwa kuhusu matatizo ya aina za uchaguzi. Kama vile *First past the post* na uwezekano wa kupata vikundi vya Wabunge wachache kutokana na kushindanisha vyama vya siasa 13 na kila kimoja kikiwa kimepata chini ya nusu ya kura zilizopigwa.

### 2.5.3 Haki na Wajibu wa Wapiga Kura

Baadhi ya wanasemina walitiwa wasiwasi na baadhi ya vyama vya siasa ambavyo viliwataka wanachama wao wajiandikishe kwenye vituo zaidi ya kimoja. Mapendekezo yalikuwa kwamba wino wa kisasa usiofutika haraka utumike.

### 2.5.4 Watumishi wa Serikali Kutokuwa na Upande

Baadhi ya wanasemina waliona kuwa hali ya kutokuwa na upande wowote kwa jeshi na viongozi wa ngazi za juu za Serikali inapingana na haki zao za binadamu za kushiriki katika uchaguzi kama wagombea wa uchaguzi.

## 2.6 Maoni ya Wataalamu Waendeshaji wa Semina

### 2.6.1 Mpango wa Elimu ya Kupiga Kura

Wanasemina waliona kuwa ufundishaji wa walimu wa elimu ya wapiga kura ukiondoa Dar es Salaam ungefanyika kabla ya zoezi la uandikishaji ili watu waweze kushaurika kujiandikisha kisha kupiga kura.

### 2.6.2 Muda Uliotengwa kwa Semina

Muda uliotengwa kwa semina ulikuwa mfupi, ukizingatia idadi ya mada za kuzungumzia. Baadhi ya wakufunzi hawakuwa na uwezo wa kufundisha mada fulani katika kitabu. Semina ya siku moja katika kiwango cha Kitaifa haikutosha kuwaelimisha watu masuala kadhaa.

### 2.6.3 Kushiriki Katika Semina

Ilishauriwa kuwa walimu wote wa shule za msingi wangeshirikishwa katika mpango wa elimu ya kupiga kura kwani wao ndio msingi mzuri wa utamaduni wa demokrasia na wanaweza kuitoa elimu yao kwa wapiga kura wengine wanaozungumza nao. Vyombo vya habari vingealikwa kwenye vituo vyote vya semina kama ilivyokuwa kwenye semina ya ngazi ya Kitaifa ili kuutangaza mpango. Ilipendekezwa pia kwamba semina zishirikishe viongozi wa vyama vya siasa katika ngazi za ufundishaji kama walivyoalikwa kwenye ngazi ya Kitaifa. Elimu kuhusu Misingi ya Demokrasia na Haki za Binadamu ilikuwa muhimu sana kwa viongozi hawa.

## 2.7 Mkutano wa Kamati ya Utendaji Mjini Lusaka

Kamati ya utendaji ya Baraza la Demokrasia ambayo ilikutana Lusaka chini ya Mwenyekiti wake Brigedia Jenerali Miyanda, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Zambia ilikuwa na agenda ifuatayo:

i) Kuzingatia maendeleo yaliyofanywa baada ya mwaka mmoja wa kazi za Baraza.

ii) Kuangalia ni kwa jinsi gani kazi za Baraza zinajulikana kwa nchi zote zinazohusika.

iii) Kufikiria njia za kupatia fedha kwa ajili ya kazi za Baraza na

iv) Kuchagua wafuatiliaji wa uchaguzi wa Tanzania, Zimbabwe na Zambia kwa uchaguzi wa mwaka 1995.

Mkutano uliridhishwa na jitihada za kuchangisha pesa, mpango wa mafunzo kwa walimu nchini Tanzania na kwa mkataba uliowekwa wa kuzitangaza kazi za Baraza. Wajumbe

walifurahishwa na toleo maalum la kijarida cha ESAURP. Walitaka Sekretariati kusambaza nakala za kijarida hicho kwa taasisi nyingi na vyama vya siasa kadri inavyowezekana.

Mwenyekiti wa mkutano alitoa ombi maalumu kwenye mkutano kuendesha mpango wa elimu ya kupiga kura nchini Zambia wakati wa uchaguzi wa mwaka 1995 huko Zambia.

### 2.8 Kufunguliwa na Kufungwa kwa Semina na Maafisa Serikali

Kitendo cha kufungua na kufungwa kwa semina na maafisa wa serikali (Wakuu wa Mikoa, Meya, Wakurugenzi wa Maendeleo (M) na (W)) kilionekana kama kitendo cha kuzithamini semina. Hotuba zote zilisisitiza umuhimu wa elimu ya uraia kwa Tanzania na kutilia mkazo zaidi kwenye elimu ya kupiga kura. Washiriki wa semina waliombwa kuchangia katika majadiliano ili kufanya semina ipate mchango toka pande zote mbili.

Hotuba nyingi wakati wa ufungaji wa semina zilisisitiza suala la wanasemina kuwa waangalifu katika kusambaza ujumbe kwa viongozi wa maoni. Washiriki walitahadharishwa wasifungamane na upande wowote wakati wa kuongea na viongozi wa maoni kwani watu hawa wana vyama vyao vya siasa.

Sura hii inamalizia kwa kusisitiza kuwa semina za walimu wa walimu ambazo zilikuwa zinaendeshwa karibu muda ule ule wa uchaguzi wa madiwani zilifanikiwa sana kulingana na idadi ya washiriki, shauku, maswali yaliyoulizwa na washiriki, maombi mengi ya kuendeleza mpango huu kwa watu wengine, kushiriki kwa wahusika (vyama vya siasa na wapiga kura) na msaada uliotolewa na Jumuiya ya Kimataifa iliopo Dar es Salaam na nje ya nchi.

Katika sura ijayo, tathmini ya athari za mafunzo kama zinavyoelezewa kwa kupitia maoni ya washiriki wa semina, inafanyika kwa kutumia njia ya kimahesabu.

SURA 3

# UFAFANUZI WA SAMPULI YA WATOA HABARI

## 3.1 Sampuli

Wakati wa mafunzo ya walimu wa walimu 98,312 dodoso 3,525 ziligawanywa kwa walimu wa Kitaifa, walimu wa Wilaya na viongozi wa maoni kwa misingi ya uwakilishi. Kwa madhumuni ya kufafanua data, makundi yaliunganishwa na kupata mawili, yaani, kundi la walimu wa kitaifa na wilaya, na kundi la viongozi wa maoni.

Wakufunzi wa kitaifa na wilaya ni wataalam, hasa walimu wa vyuo na walimu wengine ambao wamemaliza sekondari kidato cha sita na wana astashahada/stahashada au shahada. Kundi la walimu wa viongozi wa maoni ni wale wasio na shahada au stashahada lakini wanaweza kuwa na astashahada za aina fulani kufundisha. Kigezo cha msingi ni kwamba wakufunzi wawe na elimu kiasi na wawe na sifa za kiasi fulani za uongozi.

Utafiti ulipangwa katika makundi manne. Mbali na kuwa na maelezo binafsi ambayo hujumuisha jinsia, umri, elimu, ajira, kiasi cha upigaji kura, na kazi, kulikuwa pia na maswali yaliyohusiana moja kwa moja na wajihusishao na siasa: raia, vyama vya kisiasa na wapiga kura. Maswali hayo yalikuwa yanahusu nani hupiga kura na kwa nini?

Seti nyingine ya maswali ilihusu maarifa na taratibu za kujiandikisha na kupiga kura. Hasa hasa, maswali kama hayo yalikuwa yanaihusu zaidi Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Seti ya mwisho ya maswali ilihusu njia bora za kueneza elimu na habari kuhusu haki za binadamu na kuhusu taratibu za kupiga kura. Zaidi ya hayo, maswali yayo yalikuwa ni kwa faida ya Tume ya Taifa ya Uchanguzi lakini pia kwa ajili ya kuzinufaisha taasisi kama vile ESAURP ambayo inajihusisha na elimu ya demokrasia ambapo elimu ya kupiga kura ndio mafunzo muhimu.

## 3.2 Ufafanuzi wa Watoa Habari

Kati ya watoa habari 3,525, asilimia 58 walikuwa wanaume, wakati asilimia 42 walikuwa wanawake. Hiki ni kielelezo cha kutokuwepo kwa ulingano wa uongozi katika jamii ya Kitanzania kwa sababu kada ile ya kuongoza na kutoa maoni imetawaliwa na wanaume. Kwa kawaida mtu angetarajia kinyume chake: asilimia 54 wangekuwa wanawake na asilimia 46 wangekuwa wanaume kwani ndio mlingano sahihi wa idadi ya watu wa Tanzania.

Idadi ya watoa habari imetawaliwa sana na kundi la umri kati ya 22 na 55 (asilimia 87) dhidi ya wale walio na umri chini ya 22 (asilimia 6) na wale wenye umri zaidi ya 55 (angalia jedwali 1 katika kiambatisho F). Hali hii hazishangazi kwani upigaji wa kura katika Tanzania unaanzia umri wa miaka 18 na kwa hali yoyote umri wenye nguvu zaidi ni kuanzia miaka 21 hadi miaka 55. Umri wa kuacha kazi huanzia miaka 50 hadi 55.

Elimu kama tulivyoona kwenye umri, imeonyesha mwelekeo uleule kwa vile elimu ya shule ya msingi, sekondari na ufundi imepata asilimia 88 ya watoa habari wote (wakufunzi wa walimu pamoja na viongozi wa maoni). Chini ya elimu ya msingi na elimu ya juu zimepata asilimia 12. Kadhalika hakuna la kushangaza hapa ukifikiria kuwa ni asilimia 4 tu ya wanaomaliza elimu ya msingi hupata nafasi za sekondari na asilimia ndogo sana huenda vyuoni. Kwa madhumuni ya kutoa mfano, tuangalie idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu vifuatavyo: Botswana 4,000, Kenya 40,000 na Tanzania 4,000. Idadi ya watu katika nchi hizi ni Botswana milioni 1.4, Kenya milioni 25, na Tanzania milion 27. Ajira ilikuwa kipimo kingine cha kuelezea watoa habari; asilimia 55 walikuwa wameajiriwa, asilimia 23 walikuwa wamejiajiri wenyewe. Makundi yote haya mawili hufanya asilimia 78 ya watoa habari wote. Wale wasioajiriwa walikuwa asilimia 22 (angalia jedwali 2 katika kiambatisho G). Wafanyakazi wa ofisini walikuwa asilimia 53, hii ni karibu nusu ya watoa habari wote. Asilimia 32 walijitambulisha kuwa ni wakulima ambapo asilimia 10 walikuwa wafanya biashara. Watoa habari ambao ni asilimia 5, hawakuweza kutaja wako kwenye kundi gani kati ya hayo yaliyotajwa hapo juu.

Uzoefu katika kupiga kura ulikuwa pia njia nyingine ya kuelezea watoa habari: asilimia 84 ya watoa habari walikwisha wahi kupiga kura angalau mara mbili katika maisha yao na zaidi ya asilimia 11 wamewahi kupiga kura mara moja. Vilevile, takwimu hizi hazishangazi ukiangalia mambo mengine kuhusu watoa habari katika utafiti huu kama vile umri, elimu, ajira na sifa za utaalam (angalia jedwali 3 katika kiambatisho H). Kwa mchanganuo kamili wa undani kuhusu jinsia na mambo mengine (angalia jedwali 4 katika kiambatisho I).

**3.2.1** Sifa isemayo kwamba mgombea uchaguzi sharti awe "raia wa Tanzania ili asimame kwenye uchaguzi" ilipata asilimia 94 ya watoa habari 3,525. Sifa kwamba "watu wajiandikishe kwa kuorodheshwa rasmi" ilipata asilimia 92. Kuhusu kwa namna gani tutakitambua chama kilichoshinda, jibu lisemalo "Chama cha siasa chenye wagombea wengi walioshinda" ilipata asilimia 88.


Asilimia za juu zilizochagua "Chama cha siasa chenye wagombea wengi walioshinda" zimepatikana kutoka kundi la umri wa miaka kati ya 36 na 55, kundi la watoa habari wenye elimu ya sekondari, kundi la wafanyakazi wa maofisini na kundi la wale wenye uzoefu mkubwa katika kupiga kura. Kiasi cha asilimia cha watoa habari walisema kuwa "utambuzi wa chama kilichoshinda ufanywe na wafuatiliaji wa Kimataifa" kilikuwa kikubwa ukilinganisha na asilimia ya kundi ambalo limesema "halijui chama kilichoshinda kitambuliweje".

**3.2.2** Kuhusu sababu za kutopenda kujiandikisha, sababu isemayo "hakuna mabadiliko katika matokeo" ilipewa nafasi ya kwanza kati ya sababu 5 zilizotolewa yaani "kupoteza muda", "sintaki mgombea", "sikitaki chama cha siasa", na "sina muda wa kupiga kura kwa sababu nina kazi". Nafasi ya pili ilipewa sababu ifuatayo, "watu wengi wanadhani kuwa kujiandikisha huchukua muda mwingi ikiwa ni pamoja na kutembea mbali".

Katika suala hili, asilimia kubwa ya wanaume imechagua "hakuna mabadiliko katika matokeo" kuliko wanawake. Zaidi ya hayo kundi la watoa habari wenye umri kati ya (36-55) wamechagua "hakuna mabadiliko katika matokeo". Jinsi kiwango cha elimu cha watoa habari kinavyokuwa kikubwa ndivyo asilimia inavyozidi kupanda. Kwa mfano asilimia 49 imepatikana kwa wale wa chini ya elimu ya msingi na asilimia 62 kwa wale wenye elimu ya juu. Kwa mara nyingine tena, uzoefu wa kupiga kura ulihusishwa na jibu la "kutokuwa na mabadiliko". Mtoa habari mkulima katika kundi la wataalamu ndiye aliyeona kuwa kupiga kura hakutabadili chochote. Vidokezo hivi vina maana sana katika sera za Kitaifa.

**3.2.3** Sababu ya kupiga kura kama "haki ya mtu ya kikatiba" ilipata asilimia kubwa (51), kuliko sababu isemayo "ni muhimu kwa watu kuchagua viongozi wao" (Jedwali 1). Sababu ya kupiga kura kama "haki ya mtu ya kikatiba" ilipewa asilimia kubwa na wanaume kuliko wanawake, kundi la umri wa kati na wale wenye elimu ya sekondari. Kulikuwa na tofauti kubwa za asilimia kwa makundi kulingana na mahali yalipo (Dar es Salaam ikilinganishwa na sehemu nyingine ya nchi) na kwa ajira na kazi (angalia jedwali 5 na 6 katika kiambatisho J na K).

## GRAFU 1



Wanawake, wale wenye elimu ya sekondari na wale wenye umri hadi miaka 21, walitoa asilimia kubwa kwenye sababu kubwa ya pili isemayo "kupiga kura kwa ajili ya kuchagua viongozi.

Sababu ya tatu ya kupiga kura isemayo "ni kosa kuacha kupiga kura" imepata asilimia 2 tu katika sehemu ya kwanza, ikionyesha kuwa Watanzania katika mafunzo ya walimu, walielewa dhahiri kuwa kupiga kura sio kitu cha lazima na kwamba usipopiga kura huvunji sheria ya nchi (grafu 1).

### 3.3 Vigezo Changanuzi (au Vibadala)

Vionyesheo vya kupimia elimu na utaratibu wa kupiga kura vilijikita kwenye vigezo changanuzi 14 au vifungu vya data vinavyoweza kupimwa kuanzia kwenye nani ana haki ya kupiga kura na kusimama kwenye uchanguzi hadi kwenye matokeo ya uchaguzi. Kwa kila kigezo changanuzi (au vibadala) kulitolewa majibu kadhaa kwa mtoa habari ili achague jibu sahihi. Hali hii ilijitokeza kwenye maswali kama "nani anayo haki ya kusimama kwenye uchaguzi", "watu wanajiandikisha vipi," "tunakitambuaje chama kilichoshinda", "vyama vilivyoshindwa vifanye nini baada ya kushindwa" na "wapi wapeleke madai au malalamiko yao". Kwa upande wa taarifa za vipimo zilizobaki, watoa habari walitakiwa kutoa madaraja kwa majibu kadhaa yaliyotolewa, wakiyapanga kuanzia na moja(1) ikimaanisha jibu sahihi kabisa hadi tatu (3) ikimaanisha jibu la mwisho kwa usahihi. Zoezi lenyewe la kutoa madaraja linaweza kuwa chimbuko la kutoeleweka vizuri kwa swali.

Kwanza kabisa, majibu ambayo yanawezekana kuwa majibu sahihi yalitolewa. Hata majibu yote haya inawezekana yanaweza kuwa hayakuwa sahihi kwa jicho la mtoa habari. Pili, watoa habari huenda walijifikiria jibu moja sahihi zaidi na kuyaacha wazi majibu mawili yaliyobaki. Kadhalika, watoa habari wanaweza kuwa wamechagua majibu matatu ya kwanza yaliyo sahihi zaidi, na hivyo katika kufanya kosa la pili wakaruhusu kutofautiana katika kila nyanja na hivyo kurekodi namba nyingi ambazo hazipo. Kimsingi, watu wangekuwa wameulizwa kuchagua jibu sahihi zaidi miongoni mwa yote.

Kwa upande wa swali lisemalo "vyama vitakavyoshindwa vifanye nini", asilimia 78 ya watoa habari walisema kuwa vyama vilivyoshindwa lazima vikubali kushindwa na kama kuna misingi ya kulalamika basi vifuate utaratibu uliowekwa. Asilimia 87 imesema kuwa malalamiko hayo yapelekwe kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi.


**3.3.1** Kwa upande wa "sifa binafsi za mgombea uchaguzi", asilimia 92 ya watoa habari walichagua 'uwezo wa kujieleza' kama jibu la kwanza. Ni vizuri, kuzingatia kuwa "uwezo wa kujieleza" ulipendwa zaidi na wale waliosoma sana, wafanyakazi wa maofisini na wale wenye uzoefu wa kutosha wa kupiga kura. Nafasi ya pili ilichukuliwa na sifa ya "jinsia" japo kwa asilimia 4 tu. Sifa ya kabila na dini kila moja imepata asilimia 1 na nafasi ya tatu ikachukuliwa na sifa ya "umbile la mgombea".

**3.3.2** Suala la upigaji wa kura kwa misingi ya sera muhimu lilitawaliwa na "hali nzuri ya maisha" ambayo ilipata asilimia 75 ya watoa habari ambapo "ahadi za pesa na zawadi" na "vitisho" zilipewa daraja la chini. (angalia grafu 2 na jedwali 5 katika kiambatisho J).


**3.3.3** Kuhusu suala la kupiga kura kila baada ya miaka mitano, watoa habari waliona kuwa huo ulikuwa ni muda mrefu wa kutosha wa kuamua kama serikali ni nzuri katika kazi zake au la. Asilimia ya juu ilikuwa 36 ikilinganishwa na asilimia 26 iliyotolewa kwa "kuwapa wapiga kura nafasi ya kuwapigia kura viongozi wao mara kwa mara". Mambo mengine kama ile "nafasi nyingine kwa mgombea aliyeshindwa" na "kuikumbusha serikali kuhusu wajibu wake" yalipata nafasi za chini (grafu 3 na jedwali 6 katika kiambatisho J).

Wale waliotoa nafasi ya juu kwa "muda wa kutosha" ni lile kundi la umri wa miaka kati ya 36 na 55, wale walioajiriwa na wanaofanyakazi maofisini, hasa wale wasioishi Dar es Salaam na wale wenye uzoefu wa kupiga kura. Suala linalohusu "kuwapa wapiga kura nafasi nyingine ya kupiga kura" lilipewa nafasi ya juu na wafanyakazi wa maofisini, wale wenye elimu ya juu, wanaume, wakazi wa Dar es Salaam, wenye uzoefu wa kupiga kura na kundi la umri wa miaka kati ya 36 na 55. Kwa ujumla "upigaji kura wa mara kwa mara" haukupewa nafasi ya juu.

## GRAFU 2




## GRAFU 3




**3.3.4** Njia mbalimbali zilitolewa kwa watoa habari zinazohusu kujifunza habari za chaguzi ikiwa ni pamoja na: magazeti, semina, redio, kampeni za vyama vya siasa, mawakala wa serikali, vijitabu, elimu kutoka kwa ndugu na marafiki. Katika hayo redio imepata asilimia kubwa (44%) ikifuatiwa na semina (18%) na vijitabu (18%). Kupata taarifa kwa kupitia mawakala wa serikali na vyama vya siasa zilipata asilimia ndogo: asilimia 4 na 2 (Grafu 4).

## GRAFU 4




Ujumbe wa wazi hapa ni kwamba ukichanganya redio na semina na vijitabu itakuwa ni njia bora ya kuwafikia Watanzania. Kundi hili lilipata asilimia 80% ya watoa habari wote na linatoa vidokezo vya kutosha kwa wale wanaotekeleza mpango wa elimu ya demokrasia.

Asilimia kubwa zilizotolewa kwa redio zilitolewa zaidi na wanawake kuliko wanaume, na wale wenye umri wa kati kuliko kundi la wale wenye elimu kubwa, wafanyakazi maofisini, wale walio na uzoefu mkubwa wa kupiga kura, wale waishio nje ya Dar es Salaam, wale wenye uzoefu wa kupiga kura wa zaidi ya mara mbili, wakulima, waliojiajiri wenyewe na kundi la wale wenye elimu ya sekondari na ufundi.

Vijitabu juu ya demokrasia vilipewa asilimia kubwa hasa na wanaume, watoa habari wenye umri hadi miaka 21, wale wenye elimu ya msingi au chini yake, waliojiajiri wenyewe, wakulima, wale wenye uzoefu wa kupiga kura na wakazi wa Dar es Salaam (hali hii inaweza kuwa imeathiriwa na usambazaji mzuri wa vijitabu uliofanywa na ESAURP mjini Dar es Salaam).

## GRAFU 5




3.3.5 Wakufunzi wa walimu walikuwa wazi kuhusu kwa nini Tanzania inaingia kwenye mfumo wa vyama vingi. Wengi wao (70%) wanadhani kuwa "demokrasia ya vyama vingi inatoa uhuru zaidi na nafasi zaidi za kupigia kura sera, chama cha siasa na mgombea kuliko katika mfumo wa chama kimoja". Kuhusu sababu za kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi, sababu isemayo "kwenda sambamba na mwelekeo wa matukio yanayotokea kwenye nchi nyingine" ilipewa nafasi ya chini kabisa. Nafasi ya pili ilipewa sababu isemayo "haja ya kupata misaada ya kigeni" (angalia grafu 5). Sababu isemayo "uhuru kwa wapiga kura" ilipata asilimia kubwa kutoka kwa wanawake, kundi la umri kati ya miaka 36 na 55, wale waliomaliza elimu ya sekondari, walioajiriwa maofisini na wale wenye uzoefu mkubwa wa kupiga kura. Wanaume walitoa asilimia kubwa kwa sababu ya pili isemayo "Haja ya kupata misaada ya kigeni". Wengine waliotoa asilimia kubwa ni watoa habari wenye umri wa miaka 55, wale wenye elimu chini ya elimu ya msingi, wasioajiriwa, na wakulima. Hali hii hii ilirudiwa kwa nchi nyingine za Kiafrika katika kuanzisha mfumo wa vyana vingi.

3.3.6 Alama zinazohusu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi zilitolewa kwa vibadala vigezo changanuzi: hali bora ya maisha, bei nzuri ya bidhaa, kupanda kwa bei, uwezekano wa kupoteza kazi, nafasi bora za kufanya kazi na kutokuwa na uhakika juu ya kile kitakacholetwa na mfumo mpya.

Kigezo changanuzi kisemacho "kutokuwa na uhakika na yatakayotokea baadaye" kilipata silimia kubwa zaidi (45%) na kufuatiwa na kigezo kisemacho "kutokuwa na hali bora ya maisha" (angalia grafu 6).

## GRAFU 6



Kutokuwa na uhakika na mfumo wa vyama vingi ni suala la kiulimwengu kwa sasa. Kwa upande mmoja kuna hofu kuwa mfumo wa vyama vingi unaweza kusababisha kuwagawa watu na kugombea nchi. Kwa upande mwingine, inadaiwa kuwa mfumo wa vyama vingi utashawishi mashindano, kuongeza uwajibikaji na utoaji wa maoni.

Asilimia kubwa imetolewa kuhusu sababu hii kutoka kwa watoa habari wasioishi Dar es Salaam na wale wasio na uzoefu wa kutosha katika kupiga kura. Watoa habari wenye elimu chini ya elimu ya msingi hawakulipa suala hili asilimia kubwa na kulikuwa hakuna tofauti kubwa ukiangalia majibu yaliyotolewa kwa misingi ya jinsia, umri, viwango vingine vya elimu, na makundi ya ajira na kazi.

Kigezo kisemacho "tabia ya kumpigia kura mgombea yuleyule" imepata asilimia kubwa kuliko kigezo "rushwa" (ahadi ya fedha na zawadi kutoka kwa mgombea). Kwa mara nyingine tena, asilimia zilizotolewa kwa "tabia ya kumpigia kura mgombea yuleyule" imelingana kati ya sababu zinazoeleza makundi ya vigezo changanuzi. Hakuna tofauti iliyojitokeza miongoni mwa wanaume na wanawake (japo wanawake wametoa asilimia ya juu kidogo). Hata hivyo watoa habari ambao si waajiriwa, wakulima, na wale ambao hawana uzoefu wa kutosha wa kupiga kura wametoa asilimia ya chini sana (jedwali la 4 kiambatisho I).

**3.3.7** Jibu lililopata asilimia za juu kuhusu vyama vilivyoshindwa vifanye nini ni: "kukubali kushindwa" kama jambo la kwanza kufanya kisha "kufuata utaratibu katika kutoa malalamiko kama haja ipo". Jibu la "kukubali kushindwa" lilipata asilimia nyingi toka kwa wanaume, kundi la wale wenye umri kati ya miaka 36 na 55 na wale wenye elimu kubwa. Kulikuwa na tofauti ndogo ndogo miongoni mwa watoa habari wa Dar es Salaam ukilinganisha na wale walioko sehemu nyingine nchini, wale walioajiriwa na wenye kazi, wale wenye uzoefu wa kutosha wa kupiga kura na marika.

Kwa mara nyingine tena, matokeo haya yanaweza tu kudokeza uzoefu walioshakuwa nao Watanzania katika shughuli za uchaguzi.

## SURA YA 4

# MATOKEO YA UTAFITI

## 4. Ufahamu wa Hatua za Uchaguzi

Maswali kadhaa yaliulizwa ikiwa ni pamoja na: mwananchi hupata vipi habari kuhusu kujiandikisha na kupiga kura; sababu zinazoashiria watu wengine kutojiandikisha, kwa nini kuwa na uchaguzi kila mara (hususani kila baada ya miaka 5). Maswali yote yalifafanuliwa kwa vigezo au vibadala changanuzi ikiwa ni pamoja na: umri, elimu, cheo katika ajira, kazi, makazi pamoja na ni mara ngapi mtu amepiga kura (angalia viambatisho F-J).

### 4.1 Wananchi Wanavyopata Habari Kuhusu Kujiandikisha na Kupiga Kura

Watu wengi wenye umri kati ya 22 na 55 hupata habari kupitia redio na semina ikiaambatana na vijitabu. Jinsi umri unavyozidi kuwa mdogo ndivyo jinsi upashaji habari kupitia redio unavyozidi kutokuwa wa manufaa wakati ambapo mawasiliano kupitia vijitabu kuhusu demokrasia huwa muhimu. Hali ni hivyo hivyo kuhusiana na kigezo cha jinsia ingawa wanaume hujifunza kiasi kidogo zaidi kupitia redio ukilinganisha na wanawake. Hivyo hivyo wanawake hupata habari kidogo zaidi kupitia semina na vijitabu labda kutokana na wanawake kutohudhuria warsha mara kwa mara pamoja na asilimia kubwa zaidi ya wanawake kutojua kusoma na kuandika.

Kati ya wasomi, yaani wale wenye elimu ya sekondari na elimu ya juu, redio ndiyo yenye kusambaza habari zaidi kuliko njia nyingine. Hili linawiana vizuri sana na kiwango cha juu cha kipimo kinachotolewa na waajiriwa kwa redio. Hii ina maana kuwa, kuwa na kiwango cha juu zaidi cha elimu kunatoa nafasi kubwa zaidi ya kuajiriwa na papo hapo ndivyo uwezo wa kumiliki redio na kumudu betri unavyoongezeka. Vijitabu kuhusu demokrasia viliwekewa mkazo zaidi na wenye elimu ya msingi na chini yake. Hili linaeleza pia kwa nini wasioajiriwa huwekea mkazo mkubwa vijitabu. Wafanyakazi wamaofisini nao hupata habari kupitia redio zaidi kuliko wenzao wakulima na wafanyabiashara ndogo ndogo. Hata hivyo wafanyakazi na wakulima wote wanathamini sana vijitabu kuhusu demokrasia. Vijitabu vinaelekea kupendelewa vitoe habari kwa wale wenye uzoefu wa mara mbili au chini wa kupiga kura ambapo wenye uzoefu wa mara tatu na zaidi wa kupiga kura wanaelekea kupendelea kupata habari za uchaguzi kutoka kwenye redio.

Ukilinganisha mfumo wa kusambaza taarifa kwa Dar es Salaam na kwingineko inajionyesha kuwa vijitabu vinapendelewa Dar es Salaam. Kwa Dar es Salaam, hii ni kwa sababu labda kuna urahisi wa kupata vijitabu vya ESAURP. Wilaya nyingine zote zilipata vijitabu vichache. Pia asilimia kubwa ya wakazi wa Dar es Salaam wanajua kusoma na kuandika

na hii inaweza kuchangia katika kupendelea vijitabu. Hata hivyo uchunguzi zaidi unahitajika kwani Dar es Salaam ina idadi kubwa ya wakazi wake waishio nje ya mji-maeneo ya mashambani (jedwali 7 kwenye kiambatisho L).

Kuhusu njia za haraka kwa watu kujifunza kuhusu kujiandikisha kupiga kura hali ilikuwa sawa kama hapo juu: redio, semina, vijitabu. Hata hivyo wahojiwa kwenye utafiti wafikiri kuwa magazeti na vyama vya kisiasa vingeweza kuwa na ushawishi zaidi hapo baadaye.

### 4.2 Nani Wana Kaki ya Kugombea Katika Uchaguzi

Swali hili daima lilijibiwa na wengi kwa kusema kuwa ni yeyote ambaye ni Mtanzania, ambaye ana umri wa miaka 21 au zaidi, na ambaye kwa wakati huo hakuwa kifungoni. Vigezo hivi vilitajwa karibu kwa uwiano ule ule na makundi yote ya watu.

### 4.3 Jinsi Watu Wanavyojiandikisha

Kwa ujumla vigezo changanuzi kama umri, ajira, kazi na mara ngapi mtu amepiga kura havisaidii sana katika uchambuzi kwani tofauti katika kutajwa na wahojiwa mbalimbali katika utafiti siyo kubwa. Kibadala kinachodhihirisha tofauti ni elimu kwani wale wenye elimu chini ya kiwango cha elimu ya msingi walivitaja vigezo pambanuzi kwa asilimia 20 chini zaidi ya wengine na walitoa kiwango cha juu kabisa kwa kuandikisha raia kama njia mojawpo ya kujiandikisha kupiga kura.

Inaelekea wale wenye elimu ya juu zaidi ndio walielekea kusema 'kupiga kura hakutaleta tofauti sana wakiwa wanasema hivyo kwa asilimia 62 kulinganisha na asilimia 44 kwa wale wenye elimu ya chini ya kiwango cha elimu ya msingi. Vigezo changanuzi vingine havikuchanganua chochote.


### 4.4 Sababu za Kutojiandikisha Kupiga Kura

Kuhusu sababu za kutojiandikisha kupiga kura kigezo kilichotajwa cha kwanza kilikuwa kusema "hakuna mabadiliko ya matokeo". Waliosema "kupiga kura ni kupoteza muda" walifuatia kwa wingi halafu walifuatiwa na wale wenye kusema "sikumpenda mgombea". Sababu hizi mbili za mwisho zilitajwa karibu kwa mara zile zile katika nafasi ya pili (angalia grafu 7).

### 4.5 Kwa Nini Kuwa na Chaguzi Mara kwa Mara

Kama ilivyotajwa hapo nyuma, wengi walikubaliana na msemo kuwa 'miaka mitano ilikuwa muda wa kutosha kuamua kama serikali inaimudu kazi yake au hapana'. Vikundi mbali mbali katika jamii karibu vyote vilikubaliana na usemi huu bila tofauti kubwa sana kwa vigezo vya umri, ajira, kazi au mara ngapi mtu alishapiga kura. Hata hivyo wale waliosha piga kura zaidi ya mara 3 walikubaliana na msemo huu zaidi ya wengine. Wakazi

GRAFU 7




wa Dar es Salaam walikubaliana na msemo huu kidogo zaidi ya wakazi wa vijijini bila hata hivyo kuwepo tofauti kubwa katika makundi yote haya kutaja sababu kama "kuongeza uwezekano wa wapiga kura kuikumbusha serikali wajibu wake". Pia kulikuwepo tofauti zilizotokana na umri. Watu wa miaka ya kati, yaani 36 hadi 55, na wafanya kazi wa maofisini walikubaliana na msemo wa kuwa uchaguzi kila baada ya miaka 5 ilikuwa sawa. Wakulima walikubaliana na msemo huu kwa kiwango kidogo zaidi (angalia jedwali 7 katika kiambatisho L).

### 4.6 Nini Huwavutia Watu Kupiga Kura

Katika kipengee hiki mambo yafuatayo yaliangaliwa: kwa nini watu hupiga kura, ni sifa gani za mgombea binafsi huwavutia wapiga kura na ni maswala yapi huvutia wapiga kura.

#### 4.6.1 Sababu za Kupiga Kura

Watu wengi walikubaliana na msemo kuwa "ni muhimu kwa watu kupewa fursa ya kutumia haki yao ya kikatiba ya kupiga kura". Makundi mbali mbali katika jamii yalitofautiana katika kukubaliana na msemo huu. Kwa upande wa jinsia, wanaume walikubaliana na msemo huu kuliko wanawake, asilimia 53 kwa 47 kila kikundi. Kigezo cha umri kilionyesha kutajwa kwa sababu hii ya kutekeleza haki ya kikatiba.

Pia elimu zaidi, yaani sekondari na juu ya hapo, iliambatana na kuukubali msemo huu


zaidi. Hivyo hivyo elimu ya msingi ilionyesha kuwa kidogo changanuzi. Ajira, kazi, makazi na mara ngapi mtu amepiga kura hayakuwa mambo yaliyoleta tofauti kwa hili.

### 4.6.2 Sifa Kinafsi za Mgombea

Kuhusu hili wahojiwa katika utafiti hawakuonyesha tofauti zozote kwa kigezo cha jinsia, ajira au kazi. Tofauti kidogo zilijitokeza kuhusiana na misingi ya elimu na umri. Kiwango cha chini cha elimu kiliambatana na asilimia ndogo ya wahusika kutaja sifa binafsi za mgombea kama sababu ya kumpa kura. Pia wale waliosha piga kura mara 3 au zaidi huko nyuma walitoa kiwango cha juu zaidi kwa asilimia kwa sifa binafsi za mgombea.

Uwezo wa mgombea kujieleza kwa makini ni sifa muhimu kwa vyama vya siasa kwani Watanzania hawaonekani kuweka umuhimu kwenye sifa za jinsia au kabila la mgombea. Jinsia inaonekana kuwa kigezo chenye ushawishi kiasi pale inapoambatana na makazi lakini ushawishi huo sio mkubwa (tazama grafu 8 na jedwali 5 katika kiambatisho L).

GRAFU 8




### 4.6.3 Maswala Yanayowasukuma Watu Kumpigia Kura Mgombea Mmoja na Kumwacha Mwingine

Mgombea kutoa matumaini ya kuinua hali za maisha ya watu lilipewa kipaumbele dhidi ya maswala kama pesa, zawadi, vitisho na mazoea. Kulikuwepo tofauti muhimu kuambatana

na makazi, kazi na ajira, jinsia na mara ngapi mhojiwa alisha shiriki chaguzi. Hata hivyo tofauti hazikuwa kubwa kwa kigezo cha elimu na umri. Wale walio kwenye umri wa ujana katika Tanzania, yaani kati ya miaka 22 na 35, walionyesha kwa asilimia kubwa kudhamini mgombea mwenye kuleta matumaini ya kuinuka kwa viwango vya maisha. Kwa upande wa elimu, ingawa tofauti haikujionyesha kati ya wale wenye elimu ya msingi na wenye elimu ya juu, wale wenye elimu chini ya ile ya msingi asilimia yao ya kukubaliana na umuhimu wa suala la kuinua viwango vya maisha ni ndogo wakati kwa asilimia kubwa ya hawa wenye elimu chini ya elimu ya msingi walionekana kutoa kipaumbele kwa maswala ya kuahidiwa pesa au zawadi nyingine. Hata hivyo tahadhari inabidi itolewe kuhusu uwezekano wa matokeo haya ya utafiti ili kutomfanya yeyote kufikiri kuwa walio na elimu ndogo ndio walio rahisi kuhongwa wakati wakulima katika utafiti huu walichagua fedha na zawadi kwa asilimia ndogo zaidi kwa vile kulikuwepo bei nzuri kwa mazao yao kitu ambacho kinainua viwango vyao vya maisha. Ikumbukwe kwamba kwa watu wa umri wa hadi miaka 21 labda kama ni wakulima, kwa kawaida watakuwa hawana ajira nje ya sekta ya kilimo (angalia jedwali 5).

### 4.7 Hatua za Uchaguzi Baada ya Uchaguzi Wenyewe Kumalizika

Maswali yaliyoulizwa chini ya kichwa hiki yalikuwa: kufahamu kuhusu chama kilichoshinda, kutaka kujua nini vyama vitakavyoshindwa vitafanya baada ya hapo pamoja na wapi malalamiko kuhusu uchaguzi yapelekwe ikiwa kujiandikisha na kupiga kura havikuwa huru na haki.

#### 4.7.1 Jinsi Gani Chama Kilichoshinda Kinavyopatikana

Wahojiwa wengi walipendelea chama kinachoshinda kiwe kile chenye wagombea waliofanya vizuri kuliko wote. Hakukuwepo tofauti kutokana na jinsia, ajira, kazi au makazi. Tofauti zilijionyesha kuhusiana na umri kwa vile wenye umri wa kati ya miaka 35 hadi 55 walionyesha upendeleo huu uliotajwa kwa asilimia kubwa zaidi ya makundi mengine ya waliohojiwa. Elimu pia ilikuwa kigezo cha tofauti kwa vile wale wenye elimu chini ya ile ya msingi walionyesha upendeleo unaozungumzwa kwa asilimia ndogo zaidi ya makundi yote. Tofauti hizi zinaweka wazi sababu za kuwepo kwa asilimia kubwa ya wafanyakazi wa maofisini kuonyesha upendeleo kwa asilimia kubwa kuliko wote (vile wengi wao lazima wawe na elimu walau ya msingi ili waajiriwe). Vile vile wale wote ambao walisha piga kura huko nyuma kwa zaidi ya mara 3 walionyesha upendeleo kwa asilimia kubwa.

#### 4.7.2 Vyama vya Siasa Vilivyoshindwa Vifanye Nini Baada ya Uchaguzi Kwisha?

"Kufuata taratibu" kutoa malalamiko ikiwa uchaguzi haukuwa huru na haki kulipewa nafasi ya juu kabisa na wahojiwa. Hakukuwa na tofauti kwa kufuata umri na makazi. Lakini tofauti zilijitokeza kwenye jinsia ambapo wanawake walisisitiza "kufuata taratibu" na wanaume walitoa nafasi ya juu kwa "kukubali kushindwa".

Walio na elimu ya sekondari na ufundi wanaelemea zaidi kwenye kufuata taratibu tofauti na walio na elimu ya juu zaidi ambao waliipa "kukubali kushindwa" nafasi ya juu zaidi kuliko kikundi chochote kile. Asilimia 50 ya upendeleo wa "kufuata taratibu" ilijitokeza kwa walioajiriwa na wafanyakazi wa maofisini.

Waliojiajiri na wachuuzi walipendelea vyama vya siasa vikubali kushindwa. Kwa ujumla wale waliosha piga kura mara 3 au zaidi viwango vyao vya asilimia ya upendeleo wowote ilikuwa kubwa zaidi ya wale ambao wamewahi kupiga kura mara moja tu.

Ikumbukwe kuwa hoja zote mbili ya 'kufuata taratibu katika kutoa malalamiko' na 'kukubali kushindwa' zilipata upendeleo kwa viwango vikubwa vya asilimia kwa kila kikundi cha wahojiwa. Kwa kiasi fulani hii inaonyesha kuwa Watanzania, kama wanavyowakilishwa na wakufunzi na viongozi wa maoni walioshiriki kwenye utafiti huu, ni watu wanaouelewa vyema mwenendo wa uchaguzi.

### 4.7.3 Malalamiko Yapelekwe Wapi Kama Uchaguzi Haukuwa Huru na wa Haki

Kupeleka malalamiko mbele ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni hoja iliyopata upendeleo mkubwa kuliko hoja nyingine zilizopendekezwa kama: kutoa taarifa kwa polisi, kwa viongozi wa dini, kwa vyombo vya habari, kwa vyama vya kisiasa au kwa Serikali. Hakukuwepo tofauti zilizoletwa na jinsia au makazi. Ila wale wenye umri mkubwa walielekea kutoa nafasi kubwa kwa hoja ya kupeleka malalamiko kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Kwa ujumla wenye elimu zaidi, waliokuwa na uzoefu zaidi wa kupiga kura na wale wenye kufanya kazi za ofisini walielekea kujua ni wapi wapeleke malalamiko yao kuliko wenye elimu kidogo, wenye uzoefu mdogo wa kupiga kura, na vijana.

## 4.8 Unafikiri ni Kwa Nini Tumebadilisha Kutoka Mfumo wa Demokrasia ya Chama Kimoja Kuingia Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi

### 4.8.1 Kwa nini Kuingia Mfumo wa Vyama Vingi?

Wengi waliegemea ile hoja inayosema kuwa mfumo wa vyama vingi hutoa nafasi pana zaidi kwa wapiga kura kuhusiana na sera, vyama na wagombea kuliko kwenye ya mfumo wa chama kimoja. Wenye umri mkubwa na wenye kuajiriwa maofisini walionyesha kuipendelea hoja hii zaidi ya makundi mengine ya waliohojiwa. Pia uzoefu katika kupiga kura uliongeza nafasi ya kuwa na mwelekeo wa kuikubali hoja iliyotajwa hapo juu.

### 4.8.2 Kutatokea Mabadiliko Gani Katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa Kuhusu Viwango vya Maisha

Wengi walionekana kutokuwa na uhakika kuhusu mfumo wa vyama vingi kuleta mabadiliko ya kuinuka kwa viwango vya maisha. Wanaume walionekana kutokuwa na uhakika kuliko wanawake. Vivyo hivyo wenye umri mkubwa walionekana kutokuwa na

uhakika kuliko wenye umri mdogo. Pia wenye elimu na walioajiriwa maofisini walionekana kutokuwa na uhakika kuliko wengineo.

Matokeo haya ya utafiti hayashangazi kwani hata kati ya wanataaluma hakuna makubaliano kuhusiana na masuala haya. Jambo la kuzungumzia hapa ni uhusiano wa karibu ambao unahusisha mfumo wa vyama vingi vya siasa na uchumi wa soko ikilinganishwa na mfumo wa uchumi wenye kudhibitiwa na dola.

Inabidi kutoa tahadhari hapa kuwa asilimia ya waliohojiwa waliochagua "kutokuwa na uhakika" ilikuwa ni 45. Asilimia 27 ya waliohojiwa walisema "hawakutegemea mabadiliko" na mpangilio wa pili wa vigezo ulionyesha asilimia 60 ya wahojiwa hawakuwa na uhakika wakati asilimia 33 walisema hawakutegemea mabadiliko yoyote. Kati ya vijana waliohojiwa, waliosema "hawakutegemea mabadiliko yoyote" walikuwa wengi zaidi kuliko wale waliosema "hawakuwa na uhakika".

## 4.9. Maoni ya Jumla Kuhusu Elimu ya Demokrasia

Kuhusiana na swali wazi lililotaka maoni ya wahojiwa kuhusu elimu ya demokrasia, asilimia 51 walikubali kuwa elimu ya demokrasia ilikuwa ni kitu muhimu sana na walitaka taasisi zote husika zijihusishe na kutoa elimu hii na lisiwe jambo linaloshughulikikwa na taasisi chache. Waliomba kuwa semina kama hizo zilizosimamiwa na ESAURP ziwe za mara kwa mara na siyo zinazotokea mara moja tu basi.

SURA YA 5

# MUHTASARI NA HITIMISHO

Katika sura hii nitajaribu kutoa muhtasari wa yote yaliyozungumzwa hadi sasa ili kumsaidia msomaji kuelewa ni kwa nini kitabu hiki kimeandikwa.

Toka mwanzo nimesema kuwa kuna maeneo matano ya utafiti yaliyokuwa muhimu kwa shughuli nzima na kwamba vielelezo vichache vya maeneo haya matano vingeweza tu kuonyesha muelekeo wa mambo kwa kinaganaga. Tafsiri itokanayo na majibu ya wahojiwa si lazima ionyeshe mwelekeo wa kila mpiga kura mmoja mmoja. Hii inatokana na kwamba wahojiwa katika utafiti huu hawakuwa walimu halisi wa wapiga kura Tanzania. Walimu wa walimu na viongozi wenye kauli ni watu kutoka kundi la viongozi na wenye sifa ya viongozi. Mpiga kura halisi wa Kitanzania ni miongoni mwa Watanzania asilimia 75 kutoka vijijini na kwa kawaida hana majukumu ya uongozi zaidi ya kuongoza familia zao.

Tahadhari nyingine yakutoa kuhusiana na utafiti huu ni kule kukataa kwa makusudi kutumia mbinu za juu sana za sayansi ya takwimu zenye kunipa uhakika zaidi juu ufafanuzi ninaoutoa. Nilihisi kuwa wasomaji walio wengi wa kitabu hiki wangeghairi kuendelea kusoma kitabu hiki kama ningewabughudhi na michezo mingi ya tarakimu na takwimu.

## 5.1 Maeneo ya Utafiti

Utafiti ulikuwa na nia ya kuyatolea maelezo mambo yaliyo katika maeneo matano yafuatayo:

i) nani hupiga kura Tanzania na kwa nini;

ii) kutoa ushahidi kuhusu ufahamu walionao Watanzania wa hatua za uchaguzi;

iii) kutafuta ni njia zipi zinaelekea kutumika zaidi kwa ufanisi za kusambaza habari kuhusu elimu ya demokrasia na hasa elimu ihusuyo mambo ya uchaguzi;

(iv) kutathmini mbinu za ufundishaji elimu ya upigaji kura na kusambaza taarifa zipatikanazo kwa watayarishaji wa programu za elimu kama hiyo ili watayarishaji wake wafanikishe kazi zao vizuri zaidi huko mbeleni.

**5.1.1** Maeneo yote matano yalifanyiwa utafiti kwa kuwahoji watu wenye ujuzi wa ndani wa manbo ya siasa. Kupitia hawa lengo lilikuwa kutafiti ni watu gani hupiga kura, wenye viwango gani vya elimu, wenye kuishi wapi au makazi, umri gani, jinsia gani, ajira na kazi gani pamoja na kujua uzoefu wao katika kupiga kura.

Habari zilizokusanywa katika uwanja huu wa utafiti zitaisaidia ESAURP katika kutayarisha programu kwa ajili ya watumishi wa vyama vya siasa na programu kwa ajili ya semina za walimu wa walimu. Vile vile hata wagombea wenyewe wenye kutafuta kupigiwa kura watafaidika na habari zitokazo katika uwanja huu.

5.1.2 Watanzania wamekuwa wakishiriki katika kupiga kura tangu wapate uhuru miaka 30 hivi iliyopita. Lakini uzoefu wao huo ulikuwa zaidi katika kuchagua mgombea mmoja kati ya wawili kutoka chama kile kile cha kisiasa. Hivyo ilionekana walikuwa wanao ufahamu wa mambo ya uchaguzi na kama walikuwa wameupoteza katika kipindi kile cha mfumo wa chama kimoja basi ESAURP iweze kutilia mkazo jambo hilo katika mipango yake ya mafunzo ya wapiga kura, hasa kwa kuzingatia wakati huu ambapo nchi inaingia katika mfumo wa vyama vingi.

5.1.3 Njia mbali mbali zimetumika katika kusambaza habari kuhusu demokrasia ya vyama vingi. Wengine wanasema redio ndio njia bora kuliko zote. Wengine wanasema watu hawana pesa za kununulia redio na kuwa hata kama wangekuwa nazo za kununua redio basi ingekuwa shida kwa wao kuweza kupata betri za redio hizo kwa vile vipato vyao ni duni sana. Zaidi ya yote watu wengine wanasema kuwa Redio Tanzania haisikiki kote nchini nje ya Dar es Salaam na kwa vyo vyote vile vipindi vyake vinatawaliwa na misimamo ya serikali.

Semina zenye vielelezo kama vijitabu vya vikaragosi (katuni) ni njia nyingine zinazotumika (zaidi ya redio). Inasemekana kuwa semina ni njia nzuri zaidi ya zote kwa vile inatoa nafasi kwa washiriki kubadilishana mawazo na kuuliza maswali mambo ambayo yanasemekana hufanikisha sana upatikanaji wa elimu. Baadhi ya watu wanasema kuwa njia hii ni nzuri zaidi kwa kuelimishana maarifa kuliko kutoa matangazo.

Njia nyingine za kupashana habari ni kupitia vyombo vya kutoa maelezo vya serikali na kupitia kampeni za vyama vya kisiasa zinazoelekezwa kwa wapiga kura. Njia hizi za kusambaza habari zilihusishwa katika utafiti huu ili kuzinufaisha taasisi zinazowajibika kisheria au kwa hiari kutoa elimu ya demokrasia.

5.1.4 Uwanja wa nne wa utafiti ulihusu swala la kiasi gani Watanzania walioanisha demokrasia na maendeleo ya kiuchumi. Je wanahisi mambo haya yanahusiana? Kama ilivyoelezwa hapo nyuma yapo maoni, hasa katika mitizamo ya nchi za magharibi, kuwa demokrasia na maendeleo ya kiuchumi ni vitu vyenye uhusiano wa karibu. Swali ni je demokrasia huhimiza maendeleo ya kiuchumi wakati wote na je maendeleo ya kiuchumi daima huzaa demokrasia?

5.1.5 Wahojiwa katika utafiti pia waliombwa kutoa maoni yao kuhusu umuhimu wa programu ya mafunzo ya walimu wa walimu. Maswali mawili yaliulizwa: kwanza ikiwa mafunzo yalikuwa muhimu na pili ikiwa ingekuwa vizuri yaendelee kutolewa. Na vigezo changanuzi vilikuwa ni pamoja na: umri, jinsia, elimu, ajira/kazi na uzoefu kwenye kupiga kura.

## 5.2 Mhutasari wa Matokeo Maalum ya Utafiti

Tokeo kubwa kuliko yote ya utafiti huu ni kuwa kuathirika kwa mambo kutokana na programu za mafunzo kutahitaji muda mwingi wa kuwepo kwa kuathirika huko. Badala ya kutafuta mahusiano ya kitakwimu kati ya wastani wa yaliyotokea na yaliyotegemewa juhudi zaidi itabidi zielekezwe kwenye vigezo visivyo vya wazi kama vile vinavyojadiliwa katika sura ya pili, ya tatu na ya nne.

Kwa kuongezea, ni vizuri kupata habari kutoka kwa waliopitia programu za mafunzo ya demokrasia kwani wanawakilisha kiasi kikubwa cha wananchi. Sura ya nne na tano inatoa takwimu kuhusu njia hii ya kupata habari.

Watanzania wanao ufahamu wa mfumo wa uchaguzi pamoja na haki zao za kiraia. Semina zimeonyesha kuwa walikuwa makini katika kutafakari juu ya maswali nyeti katika jamii yao kama vile katiba ya nchi na uongozi wa nchi yao.

Ufahamu huu wa Watanzania haushangazi kwa vile wameshiriki kwenye uchaguzi kwa miaka 30 iliyopita. Kinachoshangaza ni kiasi kikubwa cha uelewa wa Watanzania wa wapi wangeweza kupeleka malalamiko yao pale wanapohisi haki haikutendeka katika uchaguzi.

Utafiti huu unaonyesha jinsi Watanzania wasivyokuwa na uhakika kuhusu jinsi gani mfumo wa vyama vingi utaathiri maisha yao ya kawaida. Vile vile walionyesha kutokuwa na uhakika kuhusu mahusiano kati ya mfumo wa vyama vingi na maendeleo ya kiuchumi. Inapendekezwa kuwa serikali iandae mipango madhubuti yakuiwezesha jamii ya Watanzania kushiriki katika mjadala kuhusu maswala haya.

### 5.2.1 Nani Hupiga Kura Tanzania?

Matokeo ya utafiti yamethibitisha nani hupiga kura kwa kutumia vigezo changanuzi. Mpiga kura kwa ujumla ni: mwanamume (wazo la mkuu wa familia) kati ya umri wa 36 na 55; mwenye kiwango cha elimu cha chini ya elimu ya msingi; mwenye kutegemea kilimo kama kazi; mwenye kuishi nje ya Dar es Salaam; na mwenye uzoefu wa kupiga kura.

### 5.2.2 Kwa Nini Watanzania Hupiga Kura?

Swali hili lilijibiwa kufuatana na vigezo vitatu: kupiga kura kama haki ya kikatiba; kupiga kura kutokana na mazoea ya kupiga kura mara kwa mara; na kupiga kura kutokana na msukumo au ushawishi fulani.

Watanzania walionyesha kuelewa haki zao za kibinadamu kwa vile walielewa kuwa ingawa kupiga kura ilikuwa ni haki ya kikatiba bado walikuwa hawalazimishwi

kujiandikisha au kupiga kura kwenyewe. Pili, Watanzania waliridhika kuwa miaka mitano ilitosha kama kiwango cha upigwaji kura mara kwa mara kutathmini utendaji kazi wa serikali.

### 5.2.3 Watanzania Hutafuta Nini Wakati wa Kupiga Kura?

Katika kupigia mgombea kura Watanzania walio wengi hutafuta vitu viwili vya msingi. Sifa binafsi za mgombea na mambo yanayowakera. Kuhusu sifa binafsi za mgombea Watanzania wanapendelea mgombea mwenye kujua kujieleza vizuri na mwenye kuelewa matatizo ya wapiga kura. Mambo haya yalielekea kutajwa sana katika mahojiano kuliko vigezo kama jinsia, umri au maumbile tu ya mgombea. Kuhusu kupigia mtu kura kwa kigezo cha maswala Watanzania walionekana kujali zaidi suala la viwango vya maisha kuinuka kuliko kigezo kingine chochote, ingawa mgombea ambaye tayari ameshikilia nafasi anayogombea alionyesha kuwa na nafasi kubwa yakuchaguliwa kwa vyovyote vile. Vijana wasio na ajira walionyesha kuweza kurubuniwa na zawadi za pesa au nyinginezo. Matokeo haya ya utafiti yanaonyesha umuhimu wa kulijadili swala la wagombea binafsi.

### 5.2.4 Ni Nani Mpiga Kura Mzoefu?

Utafiti unathibitisha kuwa mpiga kura mwenye uzoefu ni mwanamume; aishiye nje ya Dar es Salaam; ambaye alikuwa mwajiriwa wa kulipwa mshahara lakini asiye na ajira kwa wakati ule; mkulima mwenye umri kati ya miaka 36 na 55 na mwenye elimu chini ya kiwango cha elimu ya msingi.

### 5.2.5 Kwa Nini Baadhi ya Watanzania Hawajiandikishi Kupiga Kura

Kuhusu sababu zinazowafanya baadhi ya Watanzania kutojiandikisha kupiga kura, wahojiwa wengi walisema kuwa watu wengine hawana imani kuwa kupiga au kutopiga kura kwao kungebadilisha lolote. Wengine walitoa sababu ya kujiandikisha kwenyewe kuonekana kuchukua muda mrefu pamoja shughuli yenyewe kuonekana kuhitaji mtu kusafiri mbali ili ashiriki.

## 5.3 Vyombo Gani vya Habari vya Kutegemewa?

Masuala mawili yalijitokeza kuhusiana na njia madhubuti za kuwafikia Watanzania wapiga kura. Swala la kwanza lilihusu jinsi watu wapatavyo taarifa kuhusu uchaguzi na wengi walionekana kutegemea redio, ikifuatiwa na magazeti halafu vijitabu. Suala la pili lilihusu njia ya kupata kuelimika kuhusu maswala mbali mbali ya msingi yaelimishayo juu ya demokrasia. Wengi walitaja redio na semina pamoja na vijitabu kama vyombo vya habari vya kutegemewa. Magazeti yalitajwa katika nafasi ya tatu. Kwa vile sasa magazeti mapya yanaanza kusambazwa nje ya Dar es Salaam hali hii labda itabadilika. Wahojiwa wengine walidhani ingekuwa vema kama vyama vya kisiasa navyo vitajihusisha na shughuli hii ya usambazwaji wa elimu kuhusu demokrasia.

## 5.4 Kwa Nini Tanzania Imeingia Kwenye Mfumo wa Vyama Vingi?

Kuhusu kwa nini Tanzania imeingia kwenye mfumo wa vyama vingi wengi walisema kuwa mfumo huu hutoa uhuru zaidi kwa wapiga kura. Kuhusu matokeo ya kuingia katika mfumo wa vyama vingi wengi hawakuwa na uhakika kuhusu tofauti zitakazo jitokeza kati ya mfumo wa zamani na mfumo mpya. Wengine walikuwa jasiri kiasi cha kusema kuwa mfumo mpya hautoleta mabadiliko yoyote.

## 5.5 Kuhusu Semina za Walimu wa Walimu

Wahojiwa wengi walifikiri kuwa semina za mafunzo ya walimu zilikuwa muhimu na zenye manufaa. Ilipendekezwa semina ziendelee na vikundi zaidi vya wengine vihusishwe.

## 5.6 Mapendekezo

Yafuatayo ni mapendekezo maalum ambayo yanaelekezwa kwa taasisi za umma na za binafsi, zinazojishughulisha na masuala ya demokrasia kwa ujumla katika Tanzania.

**5.6.1** Kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza kasi ya kutayarisha elimu ya uraia na hususani elimu ya wapiga kura. Programu zinazotayarishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaelekea hazijawafikia Watanzania walio wengi. Pendekezo hapa ni kuwa Tume iongeze bidii kutayarisha mafunzo zaidi ya aina hii wakati huo huo Tume ikiziachia taasisi nyingine zenye uzoefu katika kutoa elimu ya wapiga kura na elimu ya demokrasia kwa ujumla kuendeleza mipango hii ya mafunzo kwa niaba ya Tume. Nchi za Afrika ya Kusini, Namibia na Msumbiji zinatoa mifano ya hivi karibuni ya jinsi ya kufanikisha elimu ya wapiga kura kwa kutumia vyama na taasisi zisizo za kiserikali. Kianzio kingeweza kuwa Tume kuitisha mkutano wa wote wanaohusika na suala hili kwa njia moja au nyingine. Katika mwaka 1995 ESAURP inapanga kutayarisha semina kwa watu 500,000 watakaowahamasisha kiasi cha wapiga kura milioni 10 wanaotarajiwa.

Kikundi hiki cha watu nusu milioni ni kikubwa vya kutosha kuweza kusambaza taarifa kadhaa ambazo Tume ya Taifa ya Uchaguzi ingetamani kusambaza. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa kiasi kikubwa kama hicho cha usambazaji wa taarifa na maarifa kitakachohusisha taasisi za aina nyingi namna hii kitakuwa ni cha gharama kubwa maradufu ya zile gharama zilizotumiwa na Tume (NEC) katika kutayarisha uchaguzi wa madiwani.

**5.6.2** Inapendekezwa kuwa Tume (NEC) ianze matayarisho ya uchaguzi mapema. Vituo vya kujiandikisha kupiga kura viwe karibu na wananchi iwezekanavyo ili watu wasitembee mbali kwenda kujiandikisha. Vile vile, kila inavyowezekana kuhesabu kura kufanywe karibu na vituo vya kupiga kura.

**5.6.3** Ili Tume (NEC) iweze kutekeleza majukumu yake barabara lazima iwe na uwakilishi mpana iwezekanavyo na iwe na nyenzo za kazi na watenda kazi wakutosha na ambao wanakubalika na wengi.

**5.6.4** Vyama vya kisiasa viangalie sana sifa binafsi za wagombea wao. Wagombea wenye uwezo mkubwa wa kujieleza na wenye kujua mahitaji ya wananchi wana nafasi kubwa ya kuchaguliwa.

**5.6.5** Sera za vyama vya siasa zisizojulikana zitahitaji kampeni kabambe kuzitangaza kwa vile ni mara chache sana kwa taarifa kusambaa kirahisi kutoka vyama kwenda kwa wapiga kura wanaotegemewa.

**5.6.6** Vyama vipya vinahitaji vifaa na mafunzo mazuri ya kupanga na kutekeleza kwani bila hivyo havitatoa changamoto ya kutegemewa. Inapendekezwa hapa kuwa njia maalum na za makini ziandaliwe kuviunga vyama hivi mkono. Haitasaidia kuviunga mkono kwa maneno matupu.

**5.6.7** Vyama vya kisiasa vinaweza kuhitaji kupewa nafasi zaidi kujitangaza kwenye redio ili viwafikie wapiga kura.

**5.6.8** Vile utafiti huu umeonyesha wapiga kura wako wapi katika wingi wao, vyama vya kisiasa vinaweza kuhitaji kuelekeza nguvu za kusambaza taarifa katika makazi fulani kuliko mengine, kwa mfano kuelekeza nguvu maalum sehemu za vijijini ambapo wakulima wamedhihirisha kuwa wapiga kura wa kuaminika.

**5.6.9** Imedhirika kuwa redio, semina na vijitabu vya taarifa ni vyombo madhubuti katika kusambaza elimu kuhusu demokrasia. Redio imejipambanua kama chombo muhimu kwa kutoa matangazo. Matumizi ya vyombo kama hivi yasipendelee chama chochote.

**5.6.10** Semina na vijitabu vinaonekana kutumika kwa ukamilifu katika kutayarisha programu za elimu ya demokrasia. Redio, semina na vijitabu kwa pamoja vinapendekezwa vitumike kuwasaidia wapiga kura kuelewa umuhimu wa kupiga kura.

**5.6.11** Katika sura ya kwanza hoja imejengwa kuhusu umuhimu wa kujenga nguvu madhubuti ya watendaji makini katika ngazi ya wachunguzi wa upigaji kura wenyeji wa mahali panapohusika; inapendekezwa kwa msisitizo kuwa vikundi visivyo vya kiserikali vitakavyotenda kazi ya kuwa wafuatiliaji wa uchaguzi vipewe msaada wa kifedha. Sehemu fulani ya misaada ya wahisani kuunga mkono shughuli za uchaguzi ingeweza ikaelekezwa kwenye kuyasaidia makundi kama haya.

**5.6.12** Mapendekezo haya maalum yangeweza kutolewa kwa muhtasari kama hoja sita muhimu. Kwanza ni kule kuwa na haja ya programu kabambe ya elimu ya demokrasia hususani elimu kwa wapiga kura itakayotayarishwa na vikundi mbali mbali hasa vile visivyo vya kiserikali. Pili ni kule kuwa na haja ya kuimarisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ili iwe yenye uwakilishi mpana zaidi, yenye vitendea kazi vya kutosha, yenye uwezo, yenye kukubalika kwa wote na yenye kuonekana kuwa isiyo na upendeleo wowote. Tatu ni kule kuwa na haja ya kuviona vyama vya kisiasa ambavyo ndio kwanza vimepata uhai kamili vikijitahidi kuwa imara na makini zaidi na vyenye ushawishi mkubwa zaidi. Nne ni kule kuwa na haja ya kutafakari juu ya uwezekano wa kuruhusu wagombea binafsi kwa vile ni wazi wapiga kura wengi mara nyingi hawapigii kura chama cha mgombea bali mgombea mwenyewe binafsi. Tano ni ile haja ya kuwa na usajili wa kudumu wa wapiga kura hata kama hili litatugharimu sana kama linavyoonekana kwa kuanza. Hii inaweza kutatua matatizo yanayoweza kutokea. Sita ni ile haja ya kuangalia upya katiba ya nchi.

# Kiambatisho A

## Walioshiriki Katika Semina za Mafunzo Ngazi ya Wilaya

| JINA LA WILAYA | IDADI YA WASHIRIKI | | IDADI YA VIONGOZI WA MAONI | IDADI YA WAPIGA KURA WALENGWA | IDADI VIJITABU |
|---|---|---|---|---|---|
| | WAUME | WAKE | | | |
| 1. Arumeru | 21 | 28 | 6.247 | 145.000 | 44.000 |
| 2. Bukoba Vijijini | 22 | 20 | 6.267 | 145.000 | 44.100 |
| 3. Bukoba Mjini | 8 | 7 | 912 | 30.000 | 6.600 |
| 4. Dodoma Mjini | 13 | 12 | 3.969 | 101.000 | 28.000 |
| 5. Ilala | 20 | 21 | 6.544 | 170.000 | 46.000 |
| 6. Iringa Mjini | 7 | 8 | 1.647 | 50.000 | 11.800 |
| 7. Kibaha | 7 | 7 | 1.616 | 60.000 | 11.600 |
| 8. Kilosa | 23 | 27 | 6.830 | 170.000 | 49.000 |
| 9. Kinondoni | 35 | 41 | 12.100 | 350.000 | 85.000 |
| 10. Lindi Mjini | 12 | 8 | 807 | 30.000 | 5.700 |
| 11. Mafia | 4 | 4 | 643 | 24.000 | 4.700 |
| 12. Mbeya Mjini | 14 | 7 | 2.976 | 80.000 | 20.900 |
| 13. Mbulu | 16 | 17 | 5.274 | 131.000 | 37.000 |
| 14. Morogoro Mjini | 9 | 12 | 2.293 | 60.000 | 16.500 |
| 15. Moshi Vijijini | 25 | 2 | 6.649 | 161.000 | 46.600 |
| 16. Moshi Mjini | 6 | 12 | 1.880 | 55.000 | 13.500 |
| 17. Mtwara Mjini | 11 | 6 | 1.487 | 50.000 | 10.500 |
| 18. Muleba | 16 | 17 | 5.327 | 143.000 | 48.000 |
| 19. Musoma Mjini | 7 | 7 | 1.334 | 40.000 | 10.000 |
| 20. Mwanza Mjini | 12 | 15 | 4.329 | 110.000 | 30.500 |
| 21. Tanga Mjini | 16 | 9 | 3.639 | 90.000 | 26.500 |
| 22. Temeke | 21 | 23 | 7.981 | 221.000 | 56.000 |
| 23. Ukerewe | 10 | 12 | 3.356 | 80.000 | 24.000 |
| 24. Urambo | 15 | 13 | 3.650 | 90.000 | 26.000 |
| **Jumla** | **350** | **335** | **97,757** | **2,586,000** | **692,000** |

# Kiambatisho B

## Mashirika Wahisani

**a. Wahisani kwa Mafunzo ya 1994**

**Wahisani wa Kimataifa**

- CS - Commonwealth Secretariat
- FES - Friedrich Ebert Stiftung
- ILO - International Labour Organization
- Ireland - Irish Embassy
- Japan - Japanese Embassy
- NOVIB - Netherlands Organisation for International Development Cooperation
- Switzerland - Embassy of Switzerland
- U.K. - British High Commission
- UNICEF - United Nations Children's Fund
- USA - United States of America Embassy
- WF - Westminster Foundation

**Wahisani wa Nyumbani**

- Cooper Motors Cooperation
- EXIM Bureau de Change
- IPP - Industrial Product Promotion
- Makondeko Holdings Ltd.
- Tanzania Printing Works (Makondeko Holdings Ltd)

**b. Wahisani wa Mkutano**

- Canada - Canadian High Commission
- Commonwealth Secretariat
- FES - Friedrich Ebert Stiftung
- GCA - Global Coalition for Africa
- Ireland - Irish Embassy
- NOVIB - Netherlands Organisation for International Development
- UNDP - United Nations Development Programmes (Tanzania)
- USA - United States of America Embassy

**c. Mashirika yaliyoombwa kuhisani mipango ya 1995**

- AAI - African American Institute
- ADF - African Development Foundation

- Canada - Canadian High Commission
- Carnegie Corporation
- Commonwealth Secretariat
- Denmark - Royal Danish Embassy (DANIDA)
- FES - Friedrich Ebert Stiftung
- Finland - Embassy of Finland
- Ford Foundation
- France - Embassy of France
- GCA - Global Coalition for Africa
- Holland - Royal Netherlands Embassy
- ICCO - Interchurch Organization for Development Cooperation
- Ireland - Irish Embassy
- Japan - Japanese Embassy
- Norway - Royal Norwegian Embassy
- NOVIB - Netherlands Organisation for International Development and Co-operation
- Sweden - Embassy of Sweden
- Switzerland - Embassy of Switzerland
- U.K. - United Kingdom (ODA)
- UNDP - United Nations Development Programme
- UNESCO - United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation.
- UNICEF - United Nations Children's Fund
- USA - United States of American Embassy
- USAID - United States Agency for International Development
- Westminster Foundation.

## Kiambatisho C

**Taasisi Shiriki**

- Agents for Personal Service Overseas (APSO)
- Chuo cha Ualimu cha Morogoro
- Chuo cha ualimu Dar es Salaam
- Chuo cha Ushirika Moshi
- Institute of Social Studies, The Hague (ISS)
- Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)
- Kivukoni Academy of Social Sciences (KASS)
- Mashirika 230 yasiyo ya kiserikali
- Ofisi ya Waziri Mkuu
- School of Oriental and African Studies (SOAS)
- Taasisi ya Maendeleo na Uongozi (IDM)
- Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

- Tume ya Taifa ya Uchaguzi
- University of Portsmouth
- Vyama vya Kisiasa
- Wizara ya Elimu

## Kiambatisho D

**Machapisho Katika Uwanja wa Demokrasia**

- Arusha Report — Conference Report On Political Parties in the Transition to Multiparty Democracy.
- Cost of Peace: — Views of Political Parties On the Transition to Multiparty Democracy.
- Gaborone Report: — Report On The Inaugural Meeting of the ESAURP Council for Democracy.

## Kiambatisho E

**Mashauriano/Mikutano**

- Arusha : — NOVIB Platform meeting: Democratization Process in Tanzania and possible role of NGOs.
- Bukoba/Kagera : — ELCT NWD Voter Education Seminar 20 - 21 January, 1995.
- Cotonou - Benin: — Global Coalition for Africa Meeting : 1st -4th March 1994
- Dar es Salaam: — Workshop on Local Government Election 1994 University of Dar es Salaam 26-27 January, 1995.
- Gaborone : — Conference on African Democracy Network 2nd - 4th February 1994.
- Lusaka (Zambia): — Executive Committee of the Council for Democracy Meeting 5th November 1994.
- Moshi : — Consultation on Developing a Vision and Structure for DDC/CCT/ELCT ND 31st August 1994.
- Mozambique : — Conference on Promoting a Culture of Democracy and Human Rights in Southern Africa: 7th - 11th February 1994.
- Zimbabwe : — Victoria Falls :African Election Administrators' Colloquium - 15th - 18th November 1994.

# Kiambatisho F

## Jedwali 1: Jinsia na Vibadala Vingine

| | JINSIA NA UMRI | | | | JINSIA NA ELIMU | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kufikia 21 | 22 - 35 | 36 - 55 | Zaidi ya 55 | Chini ya Elimu ya Msingi | Elimu ya Msingi | Secondari | Elimu ya Juu |
| Mme | 5.1 | 39.8 | 45.4 | 9.6 | 8.3 | 45.6 | 41.9 | 4.2 |
| Mke | 6.3 | 47.5 | 42.5 | 3.6 | 6.3 | 49.3 | 40.3 | 3.5 |
| Wastani | 5.6 | 43.0 | 44.2 | 7.1 | 7.4 | 47.2 | 41.5 | 3.9 |

| | JINSIA NA AJIRA | | | JINSI NA KAZI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ajiriwa | Jiajiri | Bila Ajira | Mkulima | Mfanyakazi ofisini | Mfanyabiashara | Wengine |
| Mme | 49.3 | 28.7 | 22.0 | 35.5 | 47.4 | 12.1 | 5.1 |
| Mke | 62.5 | 15.1 | 22.4 | 26.8 | 61.0 | 7.5 | 4.7 |
| Wastani | 54.9 | 22.9 | 22.3 | 31.8 | 53.2 | 10.1 | 4.9 |

# Kiambatisho G

## Jedwali 2 : Data Kuhusu Watu

| UMRI | ELIMU | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Chini ya Elimu ya Msingi | Elimu ya Msingi | Sekondari | Elimu ya Juu |
| Kufikia 21 | 12.2 | 65.0 | 19.3 | 3.6 |
| 22 - 35 | 4.4 | 51.8 | 40.8 | 3.1 |
| 36 - 55 | 6.7 | 41.3 | 47.6 | 4.4 |
| Zaidi ya 55 | 27.5 | 39.7 | 26.3 | 6.5 |
| Wastani | 7.5 | 47.0 | 41.5 | 3.9 |

| | UMRI NA AJIRA | | | UMRI NA KAZI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ajiriwa | Jiajiri | Bila Ajira | Mkulima | Mfanyakazi Ofisini | MfanyaBiashara | Wengine |
| Kufikia 21 | 17.3 | 29.9 | 52.8 | 50.8 | 18.3 | 19.9 | 11.0 |
| 22-35 | 56.1 | 22.2 | 21.8 | 31.2 | 55.0 | 9.4 | 4.3 |
| 36-55 | 64.9 | 20.7 | 14.3 | 24.3 | 62.0 | 8.8 | 4.9 |
| Zaidi 55 | 15.2 | 37.0 | 47.7 | 66.8 | 13.5 | 15.6 | 4.1 |
| Wastani | 54.9 | 23.0 | 22.1 | 31.8 | 53.1 | 10.2 | 4.9 |

| | UMRI NA KIWANGO CHA MAFUNZO | | | UMRI NA MAKAZI | | UMRI NA UZOEFU KUPIGA KURA | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Taifa | Wilaya | Kata | Dar | Pengineko | Mara Moja | Mara Mbili | Mara Tatu | Zaidi ya tatu |
| Kufikia 21 | -- | 1.0 | 99.0 | 48.7 | 51.3 | 51.5 | 23.6 | 9.7 | 15.2 |
| 22 - 35 | 1.1 | 4.4 | 94.1 | 36.0 | 64.0 | 15.7 | 24.3 | 22.2 | 37.9 |
| 36 - 55 | 2.1 | 21.9 | 75.9 | 31.1 | 68.9 | 2.6 | 6.6 | 16.7 | 74.0 |
| Zaidi ya 55 | 1.6 | 1.2 | 96.8 | 32.7 | 67.3 | 6.1 | 2.9 | 10.6 | 80.0 |
| Wastani | 1.5 | 11.7 | 86.5 | 34.3 | 65.7 | 10.8 | 14.8 | 18.3 | 55.9 |

| | AJIRA NA KAZI | | | | AJIRA NA UZOEFU WA KUPIGA KURA | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mkulima | Mfanyakazi Ofisini | Mfanya Biashara | Wengine | Mara Moja | Mara Mbili | Mara Tatu | Zaidi ya tatu |
| Ajiriwa | 2.6 | 90.4 | 1.4 | 5.5 | 7.7 | 14.6 | 18.7 | 58.8 |
| Jiajiri | 53.3 | 12.0 | 31.2 | 3.5 | 9.2 | 13.8 | 20.6 | 56.4 |
| Bila Ajira | 80.4 | 4.4 | 10.3 | 4.9 | 20.9 | 16.4 | 14.9 | 47.6 |
| | 31.5 | 53.4 | 10.2 | 4.9 | 10.9 | 14.08 | 18.3 | 55.9 |

| | | ELIMU NA UMRI | | | | ELIMU NA JINSIA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufikia 21 | 22 - 35 | 36 - 55 | Zaidi 55 | Mume | Mke |
| Chini ya Elimu Msingi | Dar | 19.2 | 30.1 | 28.8 | 21.9 | 64.4 | 35.6 |
| | Kwingine | 56.3 | 23.4 | 43.6 | 27.7 | 64.7 | 35.3 |
| Elimu ya Msingi | Dar | 12.5 | 47.2 | 37.7 | 6.1 | 46.0 | 54.0 |
| | Kwingine | 5.8 | 47.2 | 41.0 | 5.9 | 60.5 | 39.5 |
| Sekondari | Dar | 2.9 | 47.5 | 45.0 | 4.5 | 47.5 | 52.5 |
| | Kwingine | 2.5 | 38.9 | 54.1 | 4.5 | 65.5 | 34.5 |
| Elimu ya Juu | Dar | 6.0 | 23.9 | 56.7 | 13.4 | 62.7 | 37.3 |
| | Kwingine | 3.0 | 42.9 | 42.9 | 10.0 | 61.4 | 38.6 |
| Wastani | Dar | | | | | 48.8 | 51.2 |
| | Kwingine | | | | | 62.8 | 37.2 |

# Kiambatisho H

## Jedwali 3: Makazi na Vibadala Vingine

| | | DAR | Kwingine |
|---|---|---|---|
| Jinsia | Mume | 48.2 | 62.7 |
| | Mke | 51.2 | 37.3 |
| Umri | Kufikia 21 | 8.0 | 4.4 |
| | 22 - 35 | 45.2 | 41.9 |
| | 36 - 55 | 40.0 | 46.4 |
| | Zaidi 55 | 6.8 | 7.3 |
| Elimu | Chini ya Msingi | 6.1 | 8.3 |
| | Msingi | 41.8 | 50.0 |
| | Sekondari | 46.5 | 36.8 |
| | Elimu ya Juu | 5.5 | 3.0 |
| Ajira | Ajiriwa | 59.7 | 52.3 |
| | Jiajiri | 20.5 | 24.2 |
| | Bila Ajira | 19.9 | 23.5 |
| Kazi | Mkulima | 17.9 | 38.9 |
| | Mfanya Kazi Afisini | 58.1 | 50.5 |
| | Mfanya Biashara | 16.1 | 7.1 |
| | Wengine | 7.8 | 3.5 |
| Uzoefu wa Kupiga Kura | Mara Moja | 16.6 | 8.0 |
| | Mara Mbili | 18.0 | 13.2 |
| | Mara Tatu | 19.3 | 17.6 |
| | Zaidi ya Tatu | 45.9 | 61.1 |

# Kiambatisho I

## Jedwari 4: Uzoefu wa Kupiga Kura Na Vibadala Vingine

| KWA JINSIA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mara Moja | Mara Mbili | Mara Tatu | Zaidi ya Tatu |
| Mume | 8.7 | 11.7 | 17.1 | 62.4 |
| Mke | 13.8 | 19.3 | 19.8 | 47.0 |
| Wastani | 10.9 | 14.9 | 18.2 | 55.9 |

| KWA KIWANGO CHA MAFUNZO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Taifa | Wilaya | Kata | Dar |
| Mume | .8 | 10.8 | 88.0 | 29.1 |
| Mke | 2.4 | 12.8 | 84.6 | 42.0 |
| Wastani | 1.5 | 11.7 | 86.5 | 34.5 |

| | ELIMU NA MAKAZI | | ELIMU NA KIWANGO CHA MAFUNZO | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Dar | Kwingine | Taifa | Wilaya | Kata |
| Chini ya Msingi | 28.2 | 71.8 | - | - | 100 |
| Msingi | 30.6 | 69.4 | - | 4.9 | 94.2 |
| Sekondari | 38.7 | 61.3 | .4 | 21.2 | 78.1 |
| Elimu ya Juu | 4.9 | 51.1 | 33.6 | 14.6 | 57.8 |
| Wastani | 34.5 | 65.5 | 1.5 | 11.7 | 86.5 |

| UZOEFU WA KUPIGA KURA NA ELIMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mara Moja | Mara Mbili | Mara Tatu | Zaidi ya Mara Tatu |
| Chini ya Msingi | 16.9 | 11.7 | 21.0 | 50.0 |
| Msingi | 11.1 | 15.8 | 19.1 | 53.9 |
| Sekondari | 9.7 | 13.9 | 16.8 | 59.6 |
| Elimu ya Juu | 8.3 | 19.7 | 18.2 | 53.8 |
| Wastani | 10.9 | 14.9 | 18.2 | 55.9 |

| | ELIMU NA AJIRA | | | ELIMU NA KAZI | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ajiriwa | Jiajiri | Bila Ajira | Mkulima | Mfanya Kazi Ofisini | Mfanyakazi | Wengine |
| Chini ya Msingi | 15.2 | 34.4 | 50.4 | 76.0 | 11.2 | 8.9 | 3.9 |
| Msingi | 41.6 | 29.2 | 29.2 | 43.6 | 41.4 | 11.8 | 3.2 |
| Sekondari | 74.8 | 14.5 | 10.7 | 13.0 | 72.6 | 8.5 | 6.0 |
| Elimu ya Juu | 74.5 | 16.1 | 9.5 | 5.2 | 67.4 | 11.9 | 15.6 |
| Wastani | 54.8 | 22.9 | 22.3 | 31.8 | 53.2 | 10.1 | 4.9 |

# Kiambatisho J

## Jedwari 5 : Sababu za Kutojandikisha; Kwa Nini Kupiga Kura; Watu Hupigia Nini Kura

| SABABU ZA KUTOJIANDIKISHA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Sababu | Nafasi | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 0 |
| Hakuna Tofauti | 54 | 12 | 9 | 25 |
| Kupoteza Muda | 15 | 24 | 12 | 49 |
| Sipendi Wagombea | 14 | 22 | 18 | 46 |
| Sipendi Vyama | 5 | 8 | 12 | 75 |
| Hakuna Nafasi | 8 | 10 | 22 | 60 |

| KWA NINI KUPIGA KURA? | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Sababu | Nafasi | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 0 |
| Haki ya Kikatiba | 51 | 25 | 9 | 15 |
| Muhimu Kuchagua Viongozi | 23 | 32 | 25 | 20 |
| Ni Kuvunja Sheria Kutopiga Kura | 2 | 4 | 14 | 80 |
| Wajulishe Viongozi Maoni | 20 | 19 | 29 | 32 |

| WATU HUPIGIA NINI KURA: SIFA BINAFSI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Sababu | Nafasi | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 0 |
| Uwezo Kujieleza | 90 | 3 | 1 | 6 |
| Umbile | 2 | 21 | 16 | 61 |
| Kabila na Ukabila | 1 | 17 | 18 | 64 |
| Dini | 1 | 4 | 10 | 85 |
| Jinsia | 4 | 28 | 23 | 45 |

| MASWALA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Sababu | Nafasi | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 0 |
| Viwango Bora vya Maisha | 75 | 11 | 3 | 11 |
| Ahadi za Pesa/Zawadi | 5 | 22 | 35 | 38 |
| Vitisho | 1 | 4 | 7 | 88 |
| Desturi Kumpigia Huyo Huyo | 13 | 36 | 20 | 31 |

# Kiambatisho K

## Jedwari 6: Makazi - Dar es Salaam Dhidi ya Kwingineko

| ELIMU NA AJIRA | | | | | | ELIMU NA KAZI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Elimu | Makazi | Ajiriwa | Jiajiri | Bila Ajira | Mkulima | Mfanyakazi Ofisini | Mfanya Biashara | Wengine |
| Chini ya Msingi | Dar | 15.2 | 34.8 | 50.4 | 76.0 | 11.2 | 8.9 | 3.9 |
| | kwingine | 13.0 | 38.9 | 48.1 | 80.1 | 9.7 | 3.2 | 3.2 |
| Msingi | Dar | 41.6 | 29.2 | 29.2 | 43.6 | 41.4 | 11.8 | 2.1 |
| | kwingine | 39.8 | 30.0 | 50.1 | 51.4 | 39.1 | 7.4 | 6.0 |
| Sekondari | Dar | 74.8 | 14.5 | 10.7 | 13.0 | 72.6 | 8.5 | 9.5 |
| | kwingine | 55.5 | 23.4 | 18.2 | 13.0 | 71.8 | 6.9 | 15.6 |
| Elimu ya Juu | Dar | 74.5 | 16.1 | 9.5 | | 67.4 | 11.9 | 13.0 |
| | kwingine | 75.5 | 15.7 | 8.6 | | 73.9 | 5.8 | 4.9 |
| Wastani | Dar | 54.8 | 22.9 | 22.3 | | 53.1 | 10.2 | 3.5 |
| | kwingine | 52.3 | 24.2 | 23.5 | | 50.4 | 7.1 | |

| ELIMU NA UZOEFU KUPIGA KURA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Elimu | Makazi | Mara Moja | Mara Mbili | Mara Tatu | Zaidi ya Mara Tatu |
| Chini Msingi | Dar | 16.9 | 11.7 | 21.7 | 50.0 |
| | Kwingine | 13.1 | 10.4 | 19.7 | 56.3 |
| Msingi | Dar | 11.1 | 15.8 | 19.1 | 53.9 |
| | Kwingine | 5.6 | 14.1 | 19.3 | 57.9 |
| Sekondari | Dar | 9.7 | 13.9 | 16.8 | 59.6 |
| | Kwingine | 5.1 | 11.8 | 15.2 | 66.9 |
| Elimu Juu | Dar | 8.3 | 19.7 | 18.2 | 53.8 |
| | Kwingine | 4.3 | 25.7 | 15.7 | 54.3 |
| Wastani | Dar | 10.8 | 14.9 | 18.2 | 56.0 |
| | Kwingine | 7.9 | 13.2 | 17.7 | 61.1 |

# Kiambatisho L

## Jedwari 7: Kwa Nini Kuwa na Chaguzi za Mara kwa Mara; Njia za Kujua Kuhusu Chaguzi

| KWA NINI KUWA NA CHAGUZI MARA KWA MARA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Sababu | Nafasi | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 0 |
| Kutoa Nafasi kwa Wagombea Walioshindwa | 13 | 12 | 20 | 53 |
| Kukumbusha Serikali na Vyama Wajibu wao | 19 | 22 | 20 | 59 |
| Kuwapa Wapiga Kura Nafasi Mara kwa Mmara | 26 | 22 | 20 | 32 |
| Muda wa Kutosha | 36 | 21 | 14 | 29 |

| JINSI YA KUPATA HABARI ZA CHAGUZI | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Njia | Nafasi | | | | | |
| | 1 | | 2 | | 3 | |
| | A | P | A | P | A | P |
| Vijitabu | 18 | (6) | 11 | (16) | 11 | 8 |
| Magazeti | 6 | (2) | 11 | (23) | 13 | 11 |
| Redio | 44 | (42) | 18 | (16) | 15 | (17) |
| Ndugu/Marafiki | 3 | (2) | 5 | (4) | 13 | (5) |
| Semina n.k. | 18 | (32) | 9 | (8) | 14 | (11) |
| Wawakilishi Serikali | 4 | | 4 | | 5 | |
| Vyama vya Kisiasa | 2 | (7) | 3 | (12) | 8 | (23) |


Kumbuka : A = Halisi P = Matashi ya Baadaye

# Kiambatisho M

## Jedwari 8: Kwa nini kuingia Mfumo wa Vyama vingi; Matokeo ya Mfumo wa Vyama Vingi

| KWA NINI KUINGIA MFUMO WA VYAMA VINGI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Sababu | Nafasi | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 0 |
| Mahitaji ya Misaada ya Nje | 12 | 24 | 30 | 34 |
| Kufuata Mwelekeo wa Matukio | 9 | 34 | 25 | 32 |
| Uhuru Zaidi kwa Wapiga Kura | 70 | 9 | 9 | 12 |

| MATOKEO YA KUINGIA MFUMO WA VYAMA VINGI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Matokeo | Nafasi | | | |
| | 1 | 2 | 3 | 0 |
| Hakuna Tofauti kwa Viwango vya Maisha | 27 | 26 | 9 | 38 |
| Bei za Kuridhisha | 11 | 10 | 11 | 68 |
| Bei Juu | 3 | 8 | 14 | 75 |
| Kupoteza Ajira | 3 | 8 | 14 | 75 |
| Nafasi Zaidi za Kazi | 4 | 7 | 6 | 83 |
| Kukosa Uhakika | 45 | 16 | 13 | 26 |



Country Tanzania

Year 1995 Language Swahili

Description Who votes ~~[illegible]~~ in Tanzania and why?

IFES developed/sponsored? __________

Kitabu hiki kinatafakari kuhusu mpiga kura wa Tanzania na ni maswala yapi humsukuma kufanya hivyo. Kitabu kinalenga katika kutujulisha kiasi cha ufahamu wa Watanzania kuhusu mfumo mzima wa chaguzi za kisiasa za vyama vingi; njia bora za kusambaza taarifa kuhusu uchaguzi na mbinu zinazofaa katika kuelimisha wananchi kuhusu demokrasia ya vyama vingi. Kitabu kinabainisha mkanganyiko ambao Watanzania walio wengi wangalinao kuhusu uwiano kati ya demokrasia ya vyama vingi na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Kimechapishwa na TEMA Publishers Co. Ltd.**
**DAR ES SALAAM**

**Kinasambazwa na Tanzania Publishing House Ltd.**
**DAR ES SALAAM**